

**ULINGANIFU WA MIDHIHIRIKO NA MATUMIZI YA KIAMBISHI “KA”
NA “KU” KATIKA LAHAJA YA KIPEMBA**

MWALIMU BAKAR ALI

**TASINIFU ILIWASILISHWA IKIWA NIUKAMILISHAJI WA BAADHI YA
MASHARTI YA DIGIRII YA M.A. KISWAHILI CHUO KIKUU
HURIA CHA TANZANIA**

2018

UTHIBITISHO

Aliyeta sahihi hapo chini anathibitisha kuwa tasnifu yenye jina “**Ulinganifu wa Midhihiriko na Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba,**” ameisoma na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutunukiwa digirii ya M.A. Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....
Dkt. Bibiana S. Komunte

(Msimamizi)

Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga, kutoa chapa, kukopia kwa njia za elektroniki au njia yoyote iwayo. Ikibidi kufanya hivyo ni lazima iwe kwa ruhusa ya maandishi kutoka kwa mmiliki wa kazi hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO

Mimi, **Mwalimu Bakari Ali** nathibitisha kuwa hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine.

.....

Sahihi

Tarehe.....

TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa watoto wangu wapendwa; Bimkubwa Mwalimu Bakar na Abuubakar Mwalimu Bakar, ili iwe chachu ya kujali elimu na kujifunza kwa bidii watapokuwa wakubwa.

SHUKURANI

Kwanza namshukuru Mungu wa walimwengu wote; muumba wa mbingu na nchi na vyote vilivyomo kwa kunipa uhai, uzima, hamu na kunipa uwezo wa kuandika hadi kukamilika kwa kazi hii.

Pia nawashukuru wale wote ambao wamechangia kwa njia moja au nyingine uendelezaji na ukamilishaji wa kazi hii. Shukurani za pekee zimuendee; msimamizi wa kazi hii (Bibiana Shauri Komunte). namshukuru kwanza kwa kukubali kuwa msimamizi wa utafiti huu, pili kwa kunielekeza na kunishauri juu ya njia bora na nzuri za kuchagua mada, kukusanya data na kuweka muundo kamili wa utafiti huu katika kipindi chote.

Aidha naushukuru uongozi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hasa kwa upande wa Kiswahili (executive mode) tawi la Pemba, zaidi Bwana Bakar Kombo Bakar kwa mchango wake mkubwa katika kufanikisha kazi hii. Shukurani zangu maalumu ziwaendee wazazi wangu wapendwa Bwana Bakari Ali na Bibi Mkwasi Khamis Hamad ambao walinilea kwa upendo na kunisomesha. Pia natoa shukurani zangu za dhati kwa wanafunzi wenzangu wote wa Fasihi na Isimu tuliosomea digrii ya M.A Kiswahili mwaka 2015/2016 kwa kunipa ushauri na kuniazima vitabu vya marejeo.

Pia natoa shukurani za moyo wangu wote kwa mama watoto wangu Bi Saada Ali Makame kwa kunipa moyo katika masomo na uvumilivu wake wakati wote wa masomo yangu. Natoa shukurani pia kwa wale wote ambao walitoa mchango wao lakini sikuwataja kutokanana uchache wa muda.

IKISIRI

Utafiti huu ulihusu Ulinganifu wa Midhihiriko na Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza ulinganifu wa midhihiriko na matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba. Ili kufikia malengo, mbinu mbalimbali za utafiti zilikusika, mbinu hizo dodoso, hojaji na uchunguzi. Kwa upande wa matokeo ya utafiti; utafiti ulieleza kwamba kuna ulinganifu wa midhihiriko na matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba, katika miundo na maumbo ya maneno. Midhihiriko hio ilibainika katika njeo, mafumbo, nafsi, viambo na tungo masharti. Utafiti uligundua mfanano na tofauti kimaumbo na kimaana baina ya viambishi vya lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu. Pia utafiti ulibaini kuwa kiambishi “ka” na “ku” kina mawanda mapana ya matumizi katika lahaja ya Kipemba kikilinganishwa na kiambishi katika Kiswahili Sanifu. Mambo kadhaa yalipendekewa kwa tafiti zijazo zitupie jicho na kuyafanyia kazi. Miongoni mwa mapendekezo hayo ni pamoja na kufanya tafiti linganishi juu ya vilahaja vya Kipemba hasa, kuandikia kazi za viambishi katika vilahaja vidogo vidogo vilivyomo katika kisiwa cha Pemba.

YALIYOMO

UTHIBITISHO	i
HAKIMILIKI.....	ii
TAMKO.....	iii
TABARUKU	iv
SHUKURANI.....	v
IKISIRI.....	vi
YALIYOMO.....	vii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xii
ORODHA YA VIFUPISHO.....	xiii
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI.....	1
1.1 Utangulizi wa Jumla.....	1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti	2
1.3 Tatizo la Utafiti.....	5
1.4 Malengo ya Utafiti.....	6
1.4.1 Lengo Kuu	6
1.4.2 Malengo Mahsusi	7
1.5 Maswali ya Utafiti	7
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	7
1.7 Mipaka ya Utafiti.....	8
1.8 Vikwazo vya Utafiti.....	8
1.9 Hitimisho	9

SURA YA PILI.....	10
MAPITIO YA KAZI TANGULIZI.....	10
2.1 Utangulizi	10
2.2 Mapitio ya Maandiko.....	11
2.2.1 Maana ya Lahaja Kiujumla.....	11
2.2.2 Aina za Lahaja	14
2.2.3 Umuhimu wa Lahaja ya Kipemba	15
2.2.4 Kiambishi katika Lahaja ya Kipemba	17
2.2.5 Aina za Kiambishi	18
2.2.6 Njia za kuunda Kiambishi	23
2.3 Mkabala wa Nadharia.....	24
2.3.1 Nadharia zinazohusu Lahaja.....	27
2.3.2 Kiunzi cha Nadharia	29
2.4 Hitimisho	30
SURA YA TATU.....	31
MBINU ZA UKUSANYAJI DATA.....	31
3.1 Utangulizi	31
3.2 Muundo wa Utafiti.....	31
3.3 Eneo la Utafiti.....	31
3.4 Walengwa wa Utafiti	31
3.5 Watafitiwa wa Utafiti/ Uteuzi wa Sampuli.....	32
3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data.....	33
3.6.1 Mbinu ya Usaili	33

3.6.2	Mbinu ya Dodoso	34
3.6.3	Mbinu ya Uchunguzi Makini.....	34
3.7	Zana za Utafiti	35
3.8	Miiko ya Utafiti	35
3.9	Hitimisho	36
SURA YA NNE		37
UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA MATOKEO YA UTAFITI.....		37
4.1	Utangulizi	37
4.2	Sababu za Kutumia Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba ...	37
4.2.1	Sababu zilizochochea Kutumia Kiambishi Kihistoria.....	38
4.2.2	Sababu za Kutumia Kiambishi “ka” na “ku” kwa Kulinda Msamiati.....	39
4.2.3	Sababu zilizochochea Kutumia “ka” kutokana na Haja ya Mawasiliano....	40
4.2.4	Sababu za Kuibuka Kiambishi kutokana na Umbali wa Kijografiya	42
4.2.5	Muhtasari	43
4.3	Athari za Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba	44
4.3.1	Athari za Mtumizi ya Kiambishi “ku” katika Mafumbo	48
4.3.2	Matumizi ya Kiambishi “ka” katika Mafumbo	48
4.4	Matumizi ya Silabi “ka” na “ku” katika Tungo Masharti	50
4.5	Makundi ya Watumiaji wa Kiambishi/Silabi “ka” na “ku”	52
4.5.1	Jinsi za Watafitiwa.....	54
4.5.2	Muhtasari	55
4.6	Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika Nyanja mbali mbali za Lahaja hii	55

4.6.1	Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” kutokana na Historia	55
4.6.2	Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika Kuendeleza Mila	57
4.6.3	Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika Mambo ya Itikadi	57
4.6.4	Muhtasari	59
4.7	Mahusiano ya Silabi “ka/ku” na Mofu zingine za Lugha	59
4.7.1	Mahusiano ya Silabi “ka” na Mofu zingine za Mzizi Mwanzoni.....	60
4.7.2	Mahusiano ya Kiambishi “ka/ku” na Mofu Zingine Katika Kuibua Dhana.....	61
4.7.3	Mahusiano katika sifa za kuambathishwa na mzizi.....	62
4.7.4	Muhtasari	64
4.8	Kuvuka mipaka kwa kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja hii	64
4.8.1	Tofauti ya Maumbo Maneno ya Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu.....	66
4.9	Hitimisho	70
SURA YA TANO		71
MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....		71
5.1	Utangulizi	71
5.2	Muhtasari wa Utafiti.....	71
5.3	Muhutajari wa Matokeo ya Utafiti	73
5.3.1	Kuchunguza Sababu za kutumia Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba.....	73
5.3.2	Athari za Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba.....	74

5.3.3	Makundi ya Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba.....	75
5.4	Hitimisho	75
5.5	Mapendekezo.....	75
5.6	Tafiti Fuatishi	76
	MAREJELEO	77
	VIAMBATISHO	80

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1:	Likionesha Sababu za Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba	38
Kielelezo Na.1.1:	Kikifafanua lahaja ilivyoundwa na kiambishi katika vijiji mbali mbali Kutokana na historia.	39
Kielelezo Na.1.2:	Kikionesha Kiambishi “ka” na “ku” kutoka vijiji mbali mbali vilivyochangia kuzalisha Msamiati.....	40
Kielelezo Na.1.3:	Kikieleza kuzuka kiambishi kutokana na umbali wa kijografia	42
Kielelezo Na.1.4:	Kikionesha Msamiati ulivyozuka kutokana na Umbali wa Kijografia	43
Jadwali Na. 2:	Likionesha mgawanyiko wa Athari za kiambishi “ka” na “ku”	44
Kielelezo Na.2.1:	Kinafafanua athari za kiambishi kiwakilishi cha Njeo	45
Kielelezo Na.2.3:	Kikionesha silabi “ka” kiwakilishi mshangao.	49
Kielelezo Na.2.4:	Kikionesha silabi “ku” kiambo.	49
Kielelezo Na.2.5:	Kikionesha silabi “ka” ikiwakilisha swali kwa kuambatishwa na mofu.	50
Kielelezo Na.2.6:	Kikionesha Silabi “ku” ikiwakilisha swali kwa kuambatishwa na mofu.	50
Kielelezo Na.2.7:	Kikionesha Kiambishi “ka” na “ku” kiwakilishi cha Kihusishi.	52
Kielelezo Na.2.8:	Kikionesha Mgawanyiko wa Majibu ya Watafitiwa.....	53
Kielelezo Na.2. 9:	Kikionesha Idadi ya Washiriki na Jinsi zao.....	54
Kielelezo Na.2.10:	Kikionesha Uhusiano wa “ka/ku” na Mofu zingine katika Sifa zao.....	62
Kielelezo Na.2. 11:	Kikionesha Maumbo Maneno yalivyodondoshwa na Kuleta Maana	66

ORODHA YA VIFUPISHO

+mpumuo	Enye Mpumuo
Dkt	Daktari
Ir	Irabu
Kons	Konsonanti
Ks.s	Kiswahili Sanifu
L.kp	Lahaja ya Kipemba
-mpumuo	Sio Mpumuo
Na	Nambari
Nk	nakadhalika

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi wa Jumla

Utafiti huu ulichunguza ulinganifu wa midhihiriko na matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba. Utafiti huu uliundwa na jumla ya sura tano kuu; Sura ya kwanza iliundwa na utangulizi, usuli wa mada, pengo la utafiti, malengo, maswali ya utafiti, umuhimu, mipaka na vikwazo vya utafiti.

Sura ya pili kwa uchache kabisa, ilikuwa na mapitio ya kazi tangulizi; utangulizi, mapitio ya kazi zilizohusu mada, maana ya lahaja, aina za lahaja, umuhimu wa lahaja, dhana ya kiambishi, matumizi ya kiambishi kwa ujumla, matumizi ya kiambishi katika lahaja ya Kipemba, kuvuka mipaka kimatumizi kwa kiambishikatika lahaja ya Kipemba, mkabala wa nadharia, Nadharia kuhusu kiambishi, Nadharia kuhusulahaja, kiunzi cha nadharia na hitimisho.

Sura ya tatu iliundwa na mbinu za utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, uteuzi wa sampuli, mbinu za kukusanya data; *hojaji, dodoso, uchunguzi*, zana za utafiti, mipaka ya utafiti na hitimisho.

Sura ya nne iliundwa na ufafanuzi wa data ambapo zilishikiliwa na sababu za midhihiriko na matumizi ya “ka” na “ku”, makundi ya watafitiwa, jinsi za watafitiwa, matumizi ya viambishi, sababu za matumizi ya “ka” na “ku”, sababu za kuzuka viambishi katika lahaja hii, mahusiano na tofauti ya viambishi hivi na mofu zingine, sababu za kutumia “ka” na “ku”, matumizi ya viambish, kufanana kwa viambishi katika maumbo maneno, kufanana katika maana.

Sura ya tano imeundwa na muhutasari wa utafiti, muhutasari wa matokeo ya utafiti, mawanda mapana ya matumizi “ka” na “ku”, athari katika jamii, athari katika lahaja.

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Hii imekuwa ni kawaida kwa kila lahaja katika lugha yoyote iwayo kuwa na msamiati, viambishi ambavyo vinaweza kutofautiana na lahaja nyigine katika lugha hiyo hiyo. Na kwa upande wa lahaja ya Kipemba ilianza kuibuka na kutumia viambishi “ka” na “ku”, takribani karne tisa na zaidi hadi sasa, ambapo inakadiriwa kuwepo kwake hapa duniani toka kuandikwa kwake lahaja hii kutokana na kuibuka kwa maandishi (usanifishaji) wa lugha Afrika hasa Tanzania ya leo. Lahaja ya Kipemba ni lugha inayopatikana kwa mkusanyiko wa vilahaja vidogo vidogo vilivyomo katika kisiwa hicho ambavyo huchangia uzalishaji wa kiambishi “ka” na “ku”, kwani ni jamii moja. Waandishi waliozungumza kuhusu mada ya utafiti huu ni pamoja na Mgullu (2004), Matinde (2004), Massamba (2011), Msanjila (2012), Mnata (2014), na wengineo wengi.

Nurse & Spear (1985) wakizungumza kuhusu lugha ya Waswahili wanasema, lugha ya Waswahili ni Kiswahili chenye kujumuisha Viswahili au Lahaja zake zikiwemo; Kijomvu (Kaskazini ya Mombasa), Kiunguja Mjini (Unguja mjini Magharibi na Kati), Kipate (Kaskazini ya Pate), Kisiu (Mji wa Siu: Kenya), Kibajuni au Kitikuu (Kaskazini ya Lamu na Kusini ya Kismayuu:Shungwaya), King’ao au Kimwani (Kilwa na Kaskazini ya Mozambique), Kimtang’ata (Tanga mjini na Pangani), Kimvita (Katikati ya Mombasa), Kiamu (Kisiwa cha Lamu), Kimrima (Mafia, Rufiji na Dar es salaam), Kimakunduchi (Kusini Unguja), Chimiini au Chimbalazi au Kibarawa (Barawa), Kitumbatu(Tumbatu na Kaskazini Unguja), Chichifundi au

Chifunzi (Kusini ya Gaza hadi Wasin; Kenya), Kingazija (Komoro) na Kipemba, Kisiwa cha Pemba Kaskazini Mashariki ambacho kilizungumzwa kwa undani kiambishi “ka” na “ku”, na kuwa mtafiti alisaidiwa na maandiko kufafanua hili.

Stigand (1915) Kipemba ni lahaja inayozungumzwa katika kisiwa cha Pemba. Inafanana sana na lahaja za zamani, ina maneno mengi yaliyochukuliwa kutoka kwa wakazi wa zamani wa visiwani. Yeye alitofautisha na kulinganisha lahaja kwa kigezo cha historia bila kuzigawa lafudhi/matamshi ya maneno mbali mbali ya lahaja zilizo zungumzwa katika kisiwa cha Pemba, kama ambavyo yaweza kubainishwa katika lahaja hii kwa sasa.

Kipacha (2002) anasema kuwa, Kiswahili ni lugha ambayo ina lahaja nyingi, wasemaji wake wengi wako katika maeneo ya Afrika Mashariki, miongoni mwa lahaja hizo ni pamoja na Kitukuu, Kipate, Chimiini, Kisiyu, Kijonvu, Kingare, Kimrima, Kiamu, Kiunguja, Kimakunduchi, Kimtang’ata, Kitumbatu, King’ao, Kingome na Kipemba.

Mwandishi hapa alizungumzia zaidi tabia ya lugha ya kuchanganya vilahaja kikiwemo Kipemba ambacho ndicho kijilugha cha mada husika, ambapo mtafiti atakwenda zaidi kuangalia ulinganifu wa midhihiriko na matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja hio, “ka” na “ku”, hutumika zaidi katika mahali maalumu kwani lahaja ni aina ya uzungumzaji unaotumiwa na kikundi cha watu aghalabu katika eneo maalumu, hutofautiana uzungumzaji wake na vikundi vingine vya lugha hio hio, moja katika matamshi msamiatina kwa nadra sarufi (Ngugi na Chacha, 2004)

Lahaja ni kilugha katika lugha inayotokana nayo lakini hutofautiana maumbo, matamshi, sarufi na msamiati na hivyo hutumiwa na watu wa kundi au eneo fulani linalojitenga kijografia au kijamii

Kwa maana hizi ndio utafiti ukasema; lahaja ya Kipemba ni mfumo lugha kamili unaopatikana kwa mkusanyiko wa vilahaja vidogo vidogo ambavyo hutofautiana lafudhi na matamshi kutokana na mipaka ya Kijografia iliyojitokeza katika kisiwa hicho, mipaka ambayo huitenga jamii moja na nyingine.

Sacleux (1909) yeye aligundua kuwa Kipemba kina lahaja ndogo ndogo nne ambazo zilibainishwa kuwa ni Kipemba cha Kusini, Kipemba cha Vitongoji Mvumoni, Kichake chake cha Chake Chake na Kimsuka Chaleni. Katika uchunguzi wake alibaini matumizi ya kiambishi “ki” kinachotumika katika Kipemba badala ya “chi”. Hivyo mwandishi alituthibitishia kiambishi katika lahaja ya Kipemba na kwamba alimpa mwanga mtafiti kubaini na kuchambua athari za kiambishi “ka” na “ku”, katika lahaja hii .

Kipemba ni lahaja ambayo inazungumzwa na Wapemba na wakaazi wa kisiwa hicho kilichopo Kaskazini Mashariki mwa Tanzania. Kipemba ni lahaja ambayo ina mfumo kamili wa lugha, imesheheni vilahaja vidogo vidogo ndani yake, ambapo kunapatikana vilahaja vidogo vidogo kama vile Kikojani, Kimwambe, Kikangagani, Kiwingwi, Kimaziwang’ombe, Kikiuyu, Kimicheweni na vinginevyo ambavyo vinashikiliana kuunda lahaja hii kwa pamoja na ndani ya vilahaja hivi kunajitokeza matumizi ya kiambishi katika maneno mengi ya maongezi katika lahaja ya Kipemba. Wakaazi wa Kisiwa cha Pemba huunda lahaja yenye vilugha vidogo vidogo

ambavyo nikama sabseti ya lahaja hii, kwa mfano, lahaja X, Y na Z zote hizi huambatana na kufanya lahaja moja kubwa **R**. Lahaja X inakutana na lahaja Y na kuchangia maongezi na zote hizi hutumia viambishi katika nyanja mbali mbali za mawasiliano.

1.3 Tatizo la Utafiti

Hii imekuwa ni kawaida kwa kiambishi kuwa na ulinganifu na pia kutofautiana kimatumizi baina ya eneo moja la neno na jingine au kati ya jamii moja na nyingine zinazotumia lugha moja. BAKIZA (2010) wakizungumzia kiambishi wamesema, kiambishi ni kipande kidogo cha neno kinachokaa upande wa kushoto wa mzizi wa neno hufanya kazi kama vile; nafsi, njeo na ngeli. Kwa mujibu wa utafiti huu kiambishi “ka” na “ku”, kitaangaliwa kama umbo (mofu) katika miundo ya maneno, maumbo hayo ni pamoja na nomino, vitenzi na msamiati mwingine. Hali hii inaonekana katika maandishi mbali mbali ambapo utafiti uliyapitia matumizi ya kiambishi katika Kiswahili Sanifu, haya ni kwa baadhi ya waandishi, ila utafiti huu baada ya kukamilika utakuwa umefafanua kwa kina midhihiriko na matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika maumbo mbali mbali ya lahaja hii. Zaidi utafiti uligusia kiambishi “ka” na “ku”, katika nafsi, njeo, kiambishi “ka” na “ku”, katika mafumbo, utamatishaji, viambo vya kitarafa na tungo masharti katika lahaja ya Kipemba. Maeneo ambayo mofu hizi kwa upana zilionekana kudhihiri katika viambajengo vya maneno katika lahaja ya Kipemba. Mfano.

Mofu za nomino

/ku/	/ka/
/ku+ti/	/ka+ti/
/da+ku/	/du+ka/

Mofu za kitenzi

/ka/	/ku/
/ka+niti/	/ku+niti/
/wa+ka+ja/	/we+ku+ja/

Kiambishi “ka” na “ku” kinaonekana kuwa na dhima sawa katika mofu awali na tamati za nomino, vile vile kiambishi “ka” na “ku” kilikuwa na dhima sawa katika mofimu nafsi na njeo katika vitenzi.

Utafiti huu uliziba pengo la kitaaluma ambalo bado halijashughulikiwa. Wataalamu walio wengi walizungumzia zaidi kiambishi “ka” na “ku” katika Kiswahili Sanifu na kwa ufinyu hasa katika ngeli. Lakini ukweli ni kwamba kiambishi “ka” na “ku” kina matumizi mengi katika lahaja ya Kipemba ukilinganisha na Kiswahili Sanifu. Kwa mfano, baadhi ya matumizi ya kiambishi y“ka” na “ku”, amekwenda zaidi katika lahaja ya Kipemba. Hivyo basi ndani ya utafiti huu imedhihirika matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” yaliyopo kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu. Vile vile “ka” na “ku” hutumika kama Silabi ambayo huambatishwa na silabi vyingine kuunda msamiati katika lahaja ya Kipemba, mathalan;

Kaa !

Akaa !

Hizi ni silabi kamili ziletazo maana kama kiambajengo chochote katika lahaja ya Kipemba. Ambapo wataalamu wengi hawakujadili jambo hili. Hivyo, katika utafiti wetu tumeona kuwa kuna haja ya kuchunguza matumizi ya “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba.

1.4 Malengo ya Utafiti

1.4.1 Lengo Kuu

Kuchunguza ulinganifu wa midhihiriko na matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba.

1.4.2 Malengo Mahsusi

- 1) Kutaja sababu za kutumia kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba.
- 2) Kubainisha athari za matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba.
- 3) Kubainisha makundi ya matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba.

1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

- i) Sababu zipi ziletazo matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba?
- ii) Je athari za matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba ni zipi ?
- iii) Je makundi ya matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba ni yapi?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti kama sayansi maalumu ya uchunguzi daima utabaki kuwa muhimu kwa jamii iliyokusudiwa. Katika uchunguzi wa lugha utafiti husaidia mambo kadhaa. Kwa upande wa utafiti huu nimuhimu kwani:-

- i) Utawasaidia wasomi na wadadisi wa lugha kubaini sababu za matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba pale ambapo watahitaji kutafuta taarifa mbali mbali juu ya kiambishi hasa wanapotaka kuandika, pia kujua eneo la kiambishi na matumizi yake.

- ii) Kuwatambulisha wazungumzaji athari za matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba kama zile za makundi, mgawiko wa kijografia nk. .
- iii) Kuwasaidia waandishi wa tafiti mbali mbali zihusuzo Kipemba kubaini makundi ya matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” yanavyoweza kudhihiri katika msamiati wa lahaja ya Kipemba.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijihusisha zaidi na ulinganifu wa midhihiriko na matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika maubo lugha ya lahaja ya Kipemba katika maeneo teule ya utafiti huu kama vile matumizi ya kiambishi “ka” na “ku”, katika nafsi, njeo, mafumbo, kiambishi “ka” na “ku”, tamati na kiambishi “ka” na “ku”, kinachojitokeza katika tungo zinazoonesha ukinzani. Aidha utafiti huu utaepuka kufafanua baadhi ya matumizi ya viambishi, utafiti hautojihusisha na uchambuzi wa baadhi ya viambishi vingine vya lahaja hii.

1.8 Vikwazo vya Utafiti

Utafiti ulikumbana na matatizo mbali mbali ambayo yalirudisha nyuma wakati wa ukusanyaji data. Miongoni mwa matatizo hayo ni pamoja na:-

- i) Ukosefu wa mashirikiano kikamilifu kwa watafitiwa kutokana na woga ,hasa tukizingatia utafiti ulifanyika katika kipindi kigumu cha *Mkwamo wa Kisiasa wa Uchaguzi Mkuu Zanzibar*. 2015 baadhi ya watafitiwa waliogopa kuhojiwa kitu chochote kwa kuhofia usalama wao.
- ii) Ugumu wa usafiri; mtafiti alishindwa kuyaenda maeneo husika, ambapo utafiti ulikusudiwa kukusanywa data; baadhi ya maeneo ilibidi kuvuka visiwa

vidogo vidogo vya Pemba kama vile kisiwa cha Kojani ambacho kimezungukwa na bahari, mara nyingi kisiwa hiki hutawaliwa nadhoruba za upepo na mawimbi ya bahari.

- iii) Ugumu wa kufanya kazi za utafiti ipasavyo hasa ikizingatiwa mtafiti yumo katika kibarua.

Hata hivyo, juhudi zilichukuliwa kuyakabili matatizo haya kwa kutumia mbinu mbadala; kutafuta watafiti wa wapya waliotoa data za uhakika, kugharamia usafiri wa kisasa ili kufikia eneo teule la utafiti badala ya kutumia mitumbwi ya kijadi, kutumia muda wa ziada wakati wa usiku ili kuepuka migongano na mwajiri.

1.9 Hitimisho

Kukamilika kwa sura hii ni mfululizo wa sura zinazofuata, sura hii imetoa picha kamili juu ya kile kilichofanyika ndani ya utafiti huu. Sura hii imeanza kwa kutoa utangulizi wa jumla, usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, pengo la utafiti, umuhimu, mipaka na vikwazo vya utafiti vilijadiliwa zaidi juu ya kiambishi katika lahaja Kipemba. Kwa hiyo utafiti huu ni muhimu sana hasa kwa watu ambao wanataka kujifunza zaidi kuhusu lahaja ya Kipemba.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya machapisho mbali mbali yaliyoandikwa ambayo yanahusiana na mada ya utafiti huu. Machapisho ambayo yametoa tafsiri/fasili mbali mbali za mapitio, maana ya lahaja, aina na umuhimu wake, dhana na matumizi ya kiambishi kwa upana wake, dhana na matumizi ya nadharia na jinsi waandishi walivyofasili. Kwa kupitia machapisho mtafiti alieleza jinsi fasili zilizomo katika vyanzo hivyo zilivyosaidia utafiti huu. Lengo lake kubwa ni kuona wataalamu mbali mbali walivyozungumzia dhana ya kiambishi na kazi zake. Kwa kufanya hivyo ugunduzi wa pengo lililokuwepo ulionekana. Jambo hili lilisaidia kuibua mawazo mapya juu ya kiambishi na kuongeza maarifa katika kuichunguza lahaja hii.

Mapitio ya kazi tangulizi ni hatua yakuyadurusu maandiko ambayo yana uhusiano wa karibu na mada inayokusudiwa kufanyiwa uchunguzi kisayansi (Thungu, 2010:278). Kimsingi mapitio ya kazi tangulizi ni jumla ya nyenzo/vyanzo ambavyo husaidia kwa njia moja au nyingine kufanikisha jambo lililokusudiwa. Utafiti huu ulipitia kazi nyingi za isimu na kubaini mambo mbali mbali yanayohusu lahaja na kiambishi kwa ujumla.

Kwa kufupisha muda wa maongezi mtafiti alitumia muda mwingi kuvipitia vyanzo vya mada lakini atataja vichache kama vile:- House, R (1967), Hartman (1972), Richard (1985), TUKI (1990), Mathews (1993), Mgullu (2001), Massamba (2011), Resan, (2012), Riro (2012) na wengineo wengi ambao wote ilikuwa dira madhubuti ya kumwelekeza mtafiti katika kukamilisha utafiti.

Kwa mujibu wa Mathews (1993) Mapitio ya kazi zinazohusu mada ni kitu kinachoangaliwa sana hufanikisha kazi itakayotafitiwa. Kwa maana hii tunaweza kutumia maandiko na kuona yaliyozungumzwa kuhusu kiambishi.

2.2 Mapitio ya Maandiko

Sehemu hii inaonesha kazi mbali mbali ambazo zimeandikwa kuhusu maana ya lahaja, aina za lahaja na umuhimu wa lahaja. Vilevile imeonesha maana ya kiambishi, aina za kiambishi “ka” na “ku”, matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” maumbo maneno na Nadharia iliyohusu mada hii.

2.2.1 Maana ya Lahaja Kujumla

Kwa mujibu wa Robinson (1981) anasema kuwa lahaja ni kijilugha cha lugha fulani kinachotumiwa na watu wachache ambacho humuwezesha msemaji wake kujipatia msamiati kutoka lugha ya asili, lakini kunabaadhi ya msamiati unaoweza kumtambulisha mtu anapotoka. Lahaja mbali mbali zimebainika kuwepo duniani bila kikomo na zote hutegemea lafudhi ya watu wenyewe. Mwandishi anaona kuwa lahaja inakuwa kutokanana msamiati wa lugha ya asili, lakini ukweli ni kwamba lahaja huwa ni lugha mchanganyiko baina ya msamiati asili na msamiati unaozuka katika jamii hiyo. Vile vile tunabaini kuwa lahaja ni kilugha cha watu wachache ambao hujitegemea kimaongezi kwa kuchanganya msamiati wa asili na lugha yao ya eneo.

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) lahaja ni tofauti ya matamshi ya wasemaji wa lugha moja waliopo katika mazingira tofauti ya ardhi ya lugha hiyo. Wao wanaitazama lahaja kama mtengano wa lugha ambao hutokea pale ambapo watu hao

wametofautiana kutokana na maeneo wanayoishi. Hawa wameiona lahaja ni kitu kinachodhihiri kimazingira bila kuangalia kwa umakini maumbo matamshi, kiambishi, toni namengineyo katika lahaja.

Lahaja ni aina fulani ya kijilugha cha lugha ambacho huzungumzwa na watu wachache, ambacho humuwezesha mmoja wao kutoa tungo sambamba na tungo za lugha inayoongelewa kawaida lahaja mbali mbali zimebainika kuwepo duniani bila kikomo nazote hutegemea lafudhi ya watu wenyewe.

Lahaja ni aina ya uzungumzaji unaotumiwa na kikundi cha watu aghalabu katika eneo maalumu, hutofautiana na uzungumzaji wa vikundi vingine vya lugha hio moja katika matamshi, msamiati, kwanadra sarufi (Ngugi na Chacha, 2004:3). Pia, lahaja inaelezwa kuwa ni kilugha katika lugha inayotokana nayo lakini hutofautiana maumbo, matamshi, sarufi na msamiati na hivyo hutumiwa na watu wa kundi au eneo fulani linalojitenga kijografia au kijamii (House, 1967:397).

Njoku (2006) anasema lahaja ni vilugha vidogo vidogo vya lugha moja ambavyo hubainika kijamii au kijiografia. Kwa kawaida lahaja za lugha moja hutofautiana katika matamshi, miundo ya sarufi na msamiati. Lahaja hutofautishwa kwakupitia vipegele vifuatavyo:

- (i) Vipengele vya sera (Lahaja rasmi na lahaja sanifu).
- (ii) Vipengele vya maoni ya wasemaji wa lugha husika.
- (iii) Vipengelele vya kijamii (Lahaja jamii na lahaja tabaka).
- (iv) Vipengele vya eneo.

Kama inavyoelezwa kuwa lahaja ni vilugha vidogo vidogo ndani ya lugha moja kubwa. Au lahaja ni aina ya lugha ambayo ni maalumu kwa eneo fulani au kwa kundi fulani la kijamii. Na kwa upande wa kiambishi hivyo hivyo yako mambo mengi ambayo yanachangia kuzuka kwa kiambishi ”ka” na “ku” katika lahaja kama maelezo ya hapo juu yanavyoonekana.

Lahaja husemwa imekuwa kutokanana mambo mawili makubwa, jambo la kwanza ni kuongezeka kwa msamiati katika lahaja husika. Jambo la pili ni kupata watumiaji wengi. Kwa kawaida watumiaji wa lahaja kila wanapokuwa wengi ndio husemwa lahaja imeenea. Msamiati kila unapoongezeka ndipo lahaja husemwa imekuwa.

Lahaja ni kilugha ambacho hutokana na lugha fulani mama, ambacho hufanana na kutofautiana kwa baadhi ya mambo ya msingi; kama vile lafudhi, msamiati, sarufi, toni (viimbo), viambishi na mengineyo mengi, yanayoweza kumfanya mtu agundue mfanano au tofauti zilizopo kati yao.

Massamba (2009; 2011) akizungumza kuhusu lahaja amesema kuwa Lahaja ni mojawapo kati ya lugha ambazo kimsingi huhesabiwa kuwa lugha moja, isipokuwa zinatofautiana katika baadhi ya vipengele fulani fulani, kama vile:- lafudhi, fonolojia, msamiati au muundo kutokana na eneo ambalo lugha huzungumzwa. Lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi. Kipemba ni mojawapo ya lahaja hizo.

Lahaja ya Kipemba ni lugha inayozungumzwa na wazawa na wajuzi wa lahaja hiyo. Lahaja hii inapatikana katika Kisiwa cha Pemba, kilichozungukwa na bahari ya Hindi mipaka yake yote minne. Kisiwa cha Pemba kipo Kaskazini Mashariki ya

Tanganyika. Wakaazi wake ni watu waliojitenga; kijografia wametengwa na maeneo mengine ya Bara la Afrika kutokanana bahari. Hivyo wana kisiwa chao, utamaduni wao, itikadi zao, mila zao na lahaja yao. Lahaja hii imetafitiwa na kuonekana ina baadhi ya viambishi ambavyo vinatumika sambamba na maumbo ya maneno yaliyomo katika lahaja hiyo ili kuibua dhana mbali mbali.

2.2.2 Aina za Lahaja

Sababu za kiisimu ambazo huzalisha lahaja mpya ni zile za kijografiya na kijamii. Utamkaji tofauti hutegemea lafudhi tofaauti ambazo hujitokeza ndani ya misemo ya watu wajamii fulani. Hivyo ndivyo ambavyo katika jamii hupatikana aina kuu mbili za lahaja, ambazo ni; Lahaja za Kijografia na Lahaja za Kijamii. Lahaja za Kijografia: hizi hutokanana mtengano wa maumbile ya ardhi kama milima, bahari, misitu, jangwa, mito, n.k.

Mgullu (2004) aliigusia lahaja ya Kipemba, aliifananisha na lahaja za kijografia, anadai kuwa ni lahaja ya kijografia na alisema Kipemba kipo Afrika Mashariki, Kaskazini na Mashariki ya Tanganyika. Kipemba ni aina yalahaja ya kijografia ambayo huzungumzwa kimaeneo. Mtafiti ameitumia dhana hii ya lahaja Kijografia ili imuwezeshe kuvifafanua viambishi mbali mbali katika lahaja hii.

Sacleux (1909) aligundua kuwa Kipemba kina lahaja ndogo ndogo nne ambazo zilibainika kuwa; *Kipemba cha Kusini*, *Kipemba cha Kivitongoji Mvumoni*, *Kichakechakecha Chake Chake* na *Kimsuka Chaleni*. Katika uchunguzi wake alibaini matumizi ya kiambishi “ki” kinachotumika katika lahaja ya Kipemba badala ya “ch”. Lahaja za kijografia ni lahaja ambazo zinazungumzwa katika maeneo mbali

mbali yaliyotengana kijografia, mfano, Kipemba katika eneo la Pemba, Kitumbatu katika eneo la Tumbatu nakadhalika, haya ni maeneo yaliyotengwa na bahari. Hizi ni aina za lahaja ambazo wazungumzaji wawili au zaidi hutofautiana matamshi au lafudhi baina yao kutokana na kutengwa na vitu kama, Mito, Bahari, Milima, Misitu, Jangwa, nakadhalika. Lahaja za kijamii hizi hutokana na vyanzo vya mtengano wa kijamii zikiwemo; kabila, dini, rika, kazi, cheo na kadhalika.

Kwa mujibu Mathooko (2007) lahaja za kijamii ni aina za lugha zinazotumiwa na watu kutegemeana na tabaka, elimu, kazi, umri au uana. Anaona kuwa lahaja hii ni yawatu wakundi moja la wakaazi ila hutofautiana lugha yao kutokana na kazi zao, kiwango cha elimu kati ya wanajamii hiyo nakadhalika. Hii ni aina ya lahaja ambapo wazungumzaji wa lugha moja hutofautiana malengo, lafudhi, matamshi na sifa nyingine ndogo ndogo kutokana na tofauti za rika, kazi, jinsi, jinsia na itikadi tofauti. Lahaja za Kiswahili zimegawika makundi mbali mbali kulinganana utokeaji wake na utamkaji wake. Hii ndio tunayoiita aina za lahaja.

Maandiko yote haya yalimsaidia mwandishi kuzama ndani ya lahaja hii na kuchunguza matumizi mbali mbali ya viambishi “ka” na “ku” huku akivihariri athari zao, makundi yao nk.

2.2.3 Umuhimu wa Lahaja ya Kipemba

Kwa mujibu wa Makala (2014) lahaja inabeba majukumu mbali mbali katika jamii. Majukumu haya vile vile yanaweza kubebwa na lugha yoyote. Majukumu hayo yanaonekana kama ifuatavyo:

- i. Kitambulisho cha jamii: Lahaja hubeba jukumu la kuitambulisha jamii pale ambapo jamii fulani inazungumza. Kwa kawaida jamii inapozungumza inaweza kutambulika. Kwa mfano, Uingereza mtu anapozungumza Kokni au Kiskotlend hutambulika kwa urahisi tabaka lake na anapotoka, vilevile hapa Africa mzungumzaji anapozungumza Kiingereza cha Africa Kusini au Kiingereza cha Ulaya hujulikana kiurahisi tu anapotoka. Kwa hiyo katika lahaja za Kiswahili mtu anapozungumza Kipemba au Kimvita hujulikana kiurahisi asili yake nk.
- ii. Jukumu la kukuza mawasiliano; Mawasiliano ni jukumu moja muhimu sana linalotekelezwa na lahaja. Lahaja hapa huonekana ni kama lugha ambapo mawasiliano yanaweza kufanyika kulingana na watu wa lahaja husika bila tatizo lolote. Kwa Wapemba mathalani huwasiliana hivyo tunasema jukumu hili katika Kipemba linatekelezwa.
- iii. Lahaja inajukumu la kuhifadhi utamaduni wa jamii husika. Hapa kizazi hadi kizazi hurithishwa utamaduni wa jamii husika na utamaduni huo huhifadhiwa kutokanana lahaja inayotumika kutoka rika moja hadi rika jingine katika jamii hiyo.
- iv. Lahaja inajukumu la kukuza na kutunza msamiati, wazungumzaji wa lahaja yoyote iwayo huwa namsamiati wao wa lugha hio unaohusu elimu, kazi, dini, imani, na mambo mengine ya maisha ya jamii hiyo.

Kwa ufupi kabisa lahaja ya Kipemba ina majukumu muhimu kama misingi mikuu ya lugha yoyote duniani ambayo ni hayo hapo juu.

2.2.4 Kiambishi katika Lahaja ya Kipemba

Wanaisimu mbali mbali wamejaribu kuzungumzia juu ya dhana ya kiambishi kwa mitazamo kadhaa, kama vile; kiambishi ni kiungo muhimu katika ukamilishaji wa ngeli za majina (Mnata :2011:148uk), kiambishi hutumika katika kujenga na kudumisha lugha (Mgullu :2009).

Besha ((2007) akizungumzia kuhusu kiambishi alisema ni kipashio kinachoonesha uhusiano uliopo kati ya sentensi msingi za lugha (yaani fonimu) inamaana maalumu katika sarufi ya lugha.

BAKIZA (2010) inaeleza kuwa kiambishi ni kipande kidogo cha neno kinachokaa upande wa kushoto wa mzizi wa neno na kudokeza dhana kama vile; nafsi, njeo na ngeli, Mgullu (2001) akieleza kuhusu kiambishi tamati alikiita mofu ya kimalizio cha kitenzi, ni mofu ambayo huekwa baada ya mzizi ili kukamilisha maana, mzizi wa kitenzi unapoekwa pamoja na kimalizio tunapata shina la kitenzi lenye mzizi pamoja na kimalizio chake. Hii ina maana kuwa shina la kitenzi = {mzizi} + {kimalizio}.

Matthews (1993) anasema kiambishi ni kijipande kidogo sana ambacho hutoa maana nyingi kulingana na mahitaji ya maumbo ya lugha mahsusi, Besha (2007) alikiita kiambishi kwa jina la mofimu na kusema, mofimu ni kipashio kinachoonesha uhusiano uliopo kati ya sauti msingi za lugha na maana maalumu katika sarufi ya lugha. Kiambishi ni kiambajengo cha neno ambacho huchukua nafasi katika uundaji wa neno hilo na hubadili au kuondoa maana kabisa, iwapo kitawekwa au kitaondolewa kama kiunzi cha neno fulani cha lugha.

2.2.5 Aina za Kiambishi

Kiambishi ni kipande cha umbo ambacho hutumiwa na wanaisimu kushughulikia lugha katika kiwango cha mofolojia, sintaksia na semantikia, kiambishi huegemezewa (huambishwa) katika mzizi wa neno. Istilahi kiambishi niangavu kwani katika lugha ya Kiswahili kuambisha ni kuegemeza au kueka kitu kimoja juu ya kingine.

Kiambishi ni umbo mojawapo katika maumbo ya maneno ambacho huhesabiwa kuwa sehemu ya umbo hilo ambapo maranyingi kuwepo/kutokuwepo kwake hukamilisha, hubadili ama kufuta maana ya umbo hilo iwapolitawekwa/litaondolewa. Uegemezwaji huo hutokea maeneo mbali mbali ya manenona kutoa athari nyingi katika lugha za ulimwenguni. Maeneo hayo ni kama vile:-

- i. Mwanzoni mwa mzizi waneno (kiambishi awali).
- ii. Katikati ya mzizi waneno (kiambishi kati) na
- iii. Mwishoni mwa mzizi wa neno (kiambishi tamati).

Kiambishi kinapojitokeza mwanzoni mwa mzizi waneno huhesabiwa kuwa ni moja ya sehemu ya neno hilo. Hiki huzalisha, hukamilisha au hukwamisha maana ya msamiati iwapo kitaondoshwa. Mara nyingi kiambishi hiki hufanya kazi kama:-

i) **Kiambishi awali cha Mofu**

Besha (2007) akizungumzia kuhusu kiambishi alikiita kwa jina la mofimu na kusema, mofimu ni kipashio kinachoonisha uhusiano uliopo kati ya sentensi msingi

za lugha, kinamaana maalumu katika sarufi ya lugha. Dhana mbali mbali za mofimu awali huchimbuka mwanzoni mwa mzizi wa neno, mfano:-

Umoja, wingi, sifa, ngeli, unominishaji, urejeshi, njeo, nafsi nk.

M -toto	M - hudokeza dhana ya umoja.
Wa -toto	Wa -hudokeza dhana ya wingi.
Wa -dau	Wa -hudokeza dhana ya wingi .
Wa - hanga	Wa -hudokeza dhana ya wingi.
U -toto	U - hudokeza dhanaya sifa.
U -toro	U - hudokeza dhana ya sifa.
Pa -le	Pa - hudokeza dhana ya ngeli.
Ku -imba	Ku - hudokeza dhana ya unominishaji.
Ku -soma	Ku - hudokeza dhana ya unominishaji.
Ka -badilika	Ka - hudokeza dhana ya nafsi.
A -likuja	A - hudokeza dhana ya nafsi.
U -linita	U - hudokeza dhana ya nafsi.
Mwe -upe	Mwe - hudokeza dhana ya vivumishi.nk.

ii) **Kiambishi awali cha Njeo**

a- ku -salimia	Ku- hudokeza dhana ya njeo.
a- ka -lima	Ka- hudokeza dhana ya njeo.
wa- ku -tania	Ku- hudokeza dhana ya njeo.
a - ku -salimia	Ku- hudokeza dhana ya njeo.
a- ka -lima	Ku- hudokeza dhana ya njeo.

iii) **Kiambishi awali cha Mahali, nafsi, Idadi/Jinsi.**

Ka- badilika;	ni kiambishi awali, kiwakilishi nafsi; ya tatu, umoja.
M-tu;	ni kiambishi awali, kiwakilishi nafsi; ya kwanza, umoja.
Wa-tu;	ni kiambishi awali, kiwakilishi nafsi; ya kwanza, wingi.
Ji-tu;	ni kiambishi awali, kiwakilishi nafsi; ya tatu, ukubwishaji.
We-tu;	ni kiambishi awali, kiwakilishi nafsi; mmiliki.
Ki-tu;	ni kiambishi awali, kiwakilishi nafsi; yatatu, umoja.

iv) **Kiambishi awali Njeo (na-me-li-ta-hu-ki)**

A- na -lima,	na -ni njeo ya wakati uliopo.
A- ta -lima,	ta - ni njeo ya wakati ujao.
A- me -lima,	me - njeo ya wakati timilifu.
A- li -lima,	li - njeo ya wakati uliopita.
Hu -lima,	hu - njeo ya wakati mazoeya.
A- ki -lima,	ki - njeo ya wakati masharti.

v) **Kiambishi awali Ngeli (pa-mu-ku).**

Pa +le	Pa - ni kiambishi kiwakilishi ngeli ya pahala
Mu +le	Mu - ni kiambishi kiwakilishi ngeli ya mahala.
Ku +le	Ku - ni kiambishi kiwakilishi ngeli ya mahala mbali.

v) **Kiambishi awali Urejeshi (cho-po-ko-lo-mo-vyo-yo)**

Ali+ cho +nipa	cho - ni kiambishi kiwakilishi urejeshi, kinarejea kitu, kitendea.
Ali+ po +kuja	po - ni kiambishi kiwakilishi urejeshi, kinarejea pahala.
Wali+ ko +enda	ko - ni kiambishi kiwakilishi urejeshi, kitendwa.

Muli+**lo**+niambia **lo**-ni kiambishi kiwakilishi urejeshi, kinarejea kitu, kitendea.nk.

Tuli+**mo**+ingia **mo**- ni kiambishi kiwakilishi urejeshi, kinarejea mahala, kitendwa.

Ali+**vyo**+leta **vyo**- ni kiambishi kiwakilishi urejeshi, kitendwa.

Wali+**yo**+sema **yo**- ni kiambishi kiwakilishi urejeshi, kitendwa.

Katika kifungu (i) tunaona kuwa kiambishi kimejitokeza kabla ya mzizi wa neno na kabla ya kiambishi chochote kilichotanguliana katika kifungu (ii) kiambishi kimejitokeza kabla ya mzizi -lim- kuwakilisha wakati ambapo kimetanguliwa na kiambishi nafsi na hivyo hivyo kifungu namba (iii) kiambishi kimejitokeza kabla ya mzizi wa neno -le-.nakadhalika.

- i) Kiambishi kati; katika lugha ya Kiswahili hakuna kiambishi cha aina hii. Ilahupatikana kwa uchache katika majina ya lugha za Ulaya hasa lugha ya Kiingereza sanasanakatika “ *irregular nouns- eg: mouse-mice, woman-women, man-men, etc*”.
- ii) Kiambishi mwishoni mwa mzizi wa neno; Hiki ni kiambishi ambacho hujitokeza baada ya mzizi wa neno nahuhesabiwa kuwa ni moja ya sehemu ya neno hilo. Kiambishi tamati huekwa kwa nia ya kuzalisha, kukamilisha maana. Kiambishi tamati hufanya kazi ya utamatishaji miishoni mwa aina kuu mbili za maneno; yaani nomino na kitenzi, ilimradi kiambishi hicho kiwe kiko mwishoni mwa mzizi. Katika nomino kiambishi tamati huambikwa/ huegemezwa baada ya kiini cha neno kuibua ndumi ya ukamilishaji.

Ama katika lugha ya Kiswahili uchunguzi unaonesha kiambishi hujitokeza katika sehemukuu mbili tu, hujitokeza mwanzoni (kiambishi awali), ambacho hujitokeza kabla na baada ya kiambishi/viambishi tangulizi lakini kabla ya mzizi wa neno. Pia hujitokeza mwishoni (kiambishi tamati) hiki ni kiambishi ambacho hujitokeza baada ya mzizi wa neno pia kiambishi/viambishi tangulizi baada ya mzizi huo, kama tulivyoeleza katika (i, ii na iii) katika maelezo ya hapo juu. Kwa uelewa zaidi ainaza viambishi na ndumi zakezimeelezwa hapachini.

Vile vile “ka” hutumika kama silabi kudokeza dhana mbali mbali katika msamiati.

Miongoni mwa dhana hizo nipamoja na:-

- a) Dhana katika mkamilisho nomino.

Mashu-ka.

Mipa-ka.

Nyara-ka

Muafa-ka.nk.

- b) Dhana katika mkamilishowa kitenzi.

Alihuzuni-ka.

Tuliandi-ka.

Watatumi-ka

Palichafu-ka.nk.

Mara nyingi aina hii ya silabi hufungamanana kitenzi halisi, ambapo kiambishi aidha hutokea mwanzoni mwa neno au baada ya kiambishi tangulizi. Mfano:

LI- wakati uliopita	ki-li-chomue-ka
ME- wakati timilifu	zi-me-angu-ka
NA -wakati uliopo	tu-na-andi-ka
TA -wakati ujao	wa-ta-wajibi-ka
HU -wakati wa mazoea	hu-ondo-ka

2.2.6 Njia za kuunda Kiambishi

Mgullu (2011) akinukuliwa na (Resani, 2014) alipofafanua kuhusu kiambishi **ku**, katika Kiswahili sanifu alisema kuwa hufanya kazi kama ngeli, alieleza matumizi ya kiambishi “ku” kuwa hufanya kazi katika nomino, ila alijikita na kufafanua juu ya matumizi ya kiambishi hiki kwenye nomino tu na kuacha baadhi ya maeneo mengine muhimu ambayo kiambishi hiki hutumika katika lugha.

Midhihiriko ya kiambishi katika lahaja hujitokeza maeneo mbali mbali ya maumbo maneno ya Kiswahili kutokanana:-

- i) **Uambishwaji wa maneno**
- ii) **Minyambuliko ya maneno**

Njia mbili hizi ndizo ambazo hutumiwa na Wanaoimamu kuzalisha maumbo ya maneno mbali mbali na dhana kadhaa za maneno katika lugha.

Uambishaji wa maneno ni uingizaji wa viambajengo vya maneno kwa nia ya ukokotoaji wa dhana nyingi zilizomo ndani ya kiambajengo cha neno ambacho huekwa mwanzoni mwa neno kuu au neno msingi.

Minyambuliko ya maneno ni uwekaji mofu zilizomo katika neno ambazo kwazo dhima mbali mbali hupatikana ndani ya kiambajengo cha neno. Dhana hizo ni kama:-

- i) Kuzalisha maneno mengi katika lugha husika. Mfano silabi “tu” /m/+tu, /u/+tu, /ki/+tu...
- ii) Kuonesha nafsi katika kitenzi. Mfano: /tu/+likula, /m/+likula, /wa/+likula...
- iii) Kuonesha ngeli katika kitenzi. mfano: /ku/+napendeza, /ku/+lisaidia..
- iv) Kuonesha umoja na wingi katika majina.mfano: /m/+tu-/wa/+tu, /m/+kate-/mi/+kate..
- v) Kuonesha urejeshi katika kitenzi.mfano: ali /po/ kuja, nili /cho/ kileta...
- vi) Kuonesha njeo katika kitenzi.mfano: a /ta/ kuja, tu /li/ muita, wa /na/ elewana...
- vii) Kuonesha ukanushi katika kitenzi.mfano: /si/ mnene, /ha/ kutaki, /hu/ mpendi

2.3 Mkabala wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Umuundo, Umuumbo imeanzishwa na Chomsky (1957). Nadharia hii hutilia maanani uwezo wa kanuni za sarufi kuzalisha sentensi nyingi zenye umbo nje na umbo ndani. Nadharia inadai kwamba matamshi ya kifonetiki pamoja na mofimu hujenga matamshi hayo, kikawaida muundo ndani kwa upande mmoja na muundo nje kwa upande mwengine hupatikana. Kanuni hii hutupatia utabiri wa wazi unaohusu utamkaji wa maumbo nje, mara tu baada ya kutambua maumbo ndani ya mofimu inayohusika. Pia ni rahisi kuitambua kanuni gani inahitajika kubadili muundo wa ndani na kupata muundo nje. Nadharia inadaiwa kuwa hufafanua lugha kwa viwango vikuu viwili ambavyo ni:-

- i. *Isimu maumbo ya minyambuliko ya maneno.*
- ii. *Isimu maumbo ya Miundo ya maneno.*

Isimu Maumbo ya minyambuliko ya maneno; hushughulikia minyambuliko ya viambajengo vya maneno, huchunguza maaumbo ya maneno na dhana zake, ni kiwango cha lugha kinachoshikiliana na fonolojia, Isimu Miumdo na Isimu Maana katika kujenga lugha. Hii ni dhana inayojishughulisha na umbo la lugha “mofu” katika upangaji na ufafanuzi wa lugha. Katika uchanganuzi wa mofu. Nadharia huzingatia misingi mikuu miwili, msingi wa maumbo na msingi wa maana, maumbo haya nisawa na yale yaliyoitwa kwa jina la kiambishi. Isimu Maumbo ya minyambuliko hutumia msingi wa uambishaji maumbo ya maneno, huuacha mzizi ukiwa patupu baada ya kudondoshwa viambishi vyake, mfano:-

i)...pig... ii)...imb... iii)...ndik... iv)...som...

Asili ya maneno haya yote ni vitenzi ambavyo vimedondoshwa viambishi vyake na kuachwa mizizi na hivyo ndivyo kazi ya ubainishaji wa kiambishi kilivyoangaliwa katika Lahaja ya Kipemba.

Isimu Miundo ya manenokwa upande mwingine, hushughulika na uchambuzi wa maneno kutoka kategoria moja ya neno kwenda nyingine kutokana na neno lile lile la asili, mfano:-

Lima- ku-lima- limiana-limisha-limiwa.nk,

Imba- ku-imba-imbiana-imbisha.nk,

Soma- ku-soma-someana.nk.

Kwa kuwa kazi hii ililenga kuchunguza umbo dogo la neno (kiambishi/silabi) mtafiti aliona ni sawa kutumia dhana ya Maumbo iliyozalikana kutokana na Nadharia ya

Umuundo. Dhanahii hii ndogo ilizalikana kutokana na uendelezaji wa Nadharia ya Umuundo ambayo ilizungumzia umbo nje na umbo ndani, dhana ya Maumbo ilisaidia utafiti huu kwa kuvihariri viambajengo vya maneno vinavyokuwemo ndani ya maneno na mabadiliko yake. Viambajengo vya maneno (mofu/viambishi) huchunguzwa ruwaza zake kulingana na mahali vilipowekwa.

Katika utafiti huu dhana ya Maumbo ilisaidia kutambua viambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba. Ambapo mabadiliko ya dhana yalipatikana kila palipotokea mabadiliko ya viambajengo vya maneno. Dhana ya Maumbo ilihusika moja kwa moja kuvichunguza viambishi hivi katika lahaja husika.

Hata hivyo, nadharia ya Umuundo kama tulivyoieleza hapo juu kwamba inahusu mifanyiko ya maombo kwa kuanesha uundaji wa maneno mapya kutokana na kupachika viambajengo kwenye maaneno (mofolojia ya minyambuliko ya maneno) na kuwakilisha dhana za kisarufi kwenye maumbo kwa kupachika mofu fulani kwenye mizizi ya maneno (mofolojia ya uambatizi) na kwamba inahusu ujifunzaji wa lugha hasa katika matamshi ya sauti za maneno. Tazama dhana ya Umilisi na Utendi za Chomsky. Nadharia hii imeenda mbali zaidi hadi ngazi ya sentensi. Nadhariya hii imetuziwa kujikita sana na lengo kuu la utafiti huu kwa kuangalia mofu “ka” na “ku” na kutufanya tubainishe pia miundo sentensi ambapo mofu hizo hujitokeza. Kumbe tunaweza kuonanwa kuwa hatukugusia suala la ugeuzi lengo linalopewa nafasi kubwa na Nadhariya ya Umuundo kama ilivyoonwa na Chomsky (1957) halikuwa kusudio la utafiti huu. Tukiri hapa kuwa Nadhariya ya Umuundo ni pana na chimbuko lake linahusishwa na mwana isimu Muundo anayejulikana sana [Ferdinand de Saussure (1857-1913)] na kuungwa mkono na wanaisimu wengi

akiwemo Jakob Son, Firth, Jones, Ulldal, Hjelmslev, Halliday (tunawataja wachache). Hivyo, sehemu ndogo ya Nadharia hii imehusishwa kwa kutumia vipengele vichache vilivyoelezwa na Chomsky .

2.3.1 Nadharia zinazohusu Lahaja

Kwa upande wa nadharia zinazohusu lahaja utafiti ulisaidiwa na Nadharia ya mchoroti wa unasaba lugha (family tree model) ya Greenberg J H (2011) na nadharia ya mawimbi (wave model) ya Johannes Schmidt (1872). Licha ya umuhimu wake, Nadharia ya Mchoroti na Nadharia ya Mawimbi hukosolewa kwa kuwa na udhaifu kadha wa kadha. Nadharia ya Mchoroti wa unasaba lugha ni kiunzi-picha kinachodai kuwa lugha zenye sifa kadhaa zinazofanana zina uhusiano na hutokanana lugha-mame moja. Nadharia hii hueleza kuwa lugha hizi zina uhusiano wa kinasaba. Nadharia hii inadai kuwa lugha-mame hiyo hugawanyika katika matawi mawili au zaidi. Baadae matawi hayo huanza kutofautiana kidogo kidogo. Mathalani, hutofautiana kwa kuwa wazungumzaji wake, huishi mbali mbali na huwasiliana kidogo sana au hawana mawasiliano kabisa. Baada ya muda, wazungumzaji wa tawi moja la lugha liliyogawanyika hawataweza kusikilizana na wazungumzaji wa tawi au matawi mengine ya lugha hiyo. Matawi haya huchukuliwa kuwa ni lugha tofauti kabisa. Hivyo basi, mabadiliko ya lugha-mame hii husababisha kutokea kwa lugha binti/vizalia.

Nadharia ya Mawimbi

Nadharia ya Mawimbi ni kiunzi kinachoelezea mabadiliko ya lugha ambacho kilibuniwa na Johannes Schmidt (1872) ili kushughulikia upungufu uliojitokeza katika Nadharia yamchoroti wa unasaba lugha. Yeye anachukulia kuwa mabadiliko

ya lugha husababishwa na makusano ya lugha ambapo nduni za lugha mbili zinazokusa na huchanganyika matokeo yake, lugha hizo huanza kubadilika kupoteza hali yake ya awali.. Hii hufuatiwana kuibuka kwa lahaja na baada ya mabadiliko kufanyika polepole kwa miaka mingi, lahaja hizi huwa lugha zinazojitegemea. Nadharia ya Mawimbi imeweza kujibu baadhi ya maswali yaliyosababisha kukosolewa kwanadharia ya mchoroti wa unasaba lugha. Baadhi ya majibu hayo ni moja, nadharia ya mawimbiimeweza kuonesha sababu ya kugawanyika kwa lugha-mame na kutokea kwa lugha binti/vizalia. Katika kushughulikia suala hili, nadharia ya Mawimbi inatambua kuwa makusano ya lugha na mgawanyiko wa lugha huchombeza kutokea kwa mabadiliko ya lugha.

Hii hufuatiwa na kuzuka kwa lahaja na baada ya mabadiliko kufanyika pole pole kwa miaka mingi lahaja hizi huwa lugha zinazojitegemea. Nadharia hii ilisaidia utafiti huu katika kujua uibukaji na matumizi ya viambishi katika lahaja ya Kipemba kwenye misamiati mbali mbali ya lugha husika.

Dhana hii inaunganisha dhana zilizoelezwa katika nadharia mbili za kimapokeo (Nadharia yamchroti wa unasaba lugha na Nadharia ya mawimbi) kwa misingi ifuatao:


Kwanza, inatambua kuwa makusano ya lugha husababisha kusambaa kwa nduni za lugha moja kwenda lugha nyingine.

Pili, mabadiliko ya asili ambapo lugha moja hugawanyika na kuzaa lugha kadhaa wakati wa kuingiliwa ghafla na lughu. Hivyo basi, lugha ambayo inaaminiwa kuwa

imezaa lugha nyingine huitwa lugha-mame. Lugha zilizozaliwa na lugha-mame huitwa lugha binti; lugha vizalia vya lugha mame hii.

2.3.2 Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ya Ummundo ya Chomsky (1957) tukiutumia dhana ndogo mbili, Dhana ya Maumbo na Dhana ya Miundo ya maneno, hutupa kiunzi picha cha umbo la kiambajengo cha neno ambapo kuna taswira kama ya kiowevu. Kiowevu kilichoundwa kwa vipande vidogo vidogo vilivyowekwa pamoja hadi kufikia kitu kamili imefanana na taswira ya jengo lililowekwa vipande vidogo vidogo vya matofali sawa na viambajengo/kiambishi “ka” na “ku”, /maumbo lugha yaliyotoka kila kona na kujitupa pamoja kuunda neno. Kwa mfumo huo hujengwa dhana, kwa kuivuta taswira ya kiambajengo katika lahaja ya Kipemba ambayo kidogo kidogo ilianza kukua na kukua hadi kufikia mithili ya umbo (neni) kamili huku likisheheni silabi zilizoundwa kutokana na viambishi mbali mbali. Katika mchoro huu kuna usilisila wa maneno ya lahaja ya Kipemba ambayo yameathiriwa na “ka” na “ku” ambapo makundi mbali mbali ya maneno yalijiunga kwa pamoja na kutoa mchango wa kuwepo kwa lahaja hiyo. Kama ilivyo elezwa hapo awali kuwa viambajengo vya maneno viliungana pamoja na kuunda neno katika lahaja ya (KIPEMBA).



Chanzo: Mchoro wa Nadharia (Mgullu, 2001)

2.4 Hitimisho

Ukamilikaji wa sura hii ni mfululizo wa sura nyingine, sura hii ni jumla ya mapitio ya kazi tangulizi zilizohusu mada, maana ya lahajana kiambishi, matumizi ya kiambishi katika lahaja ya Kipemba, mkabalawa Nadharia na Nadharia zilizohusu kiambishi, nadharia zilizohusu lahaja na kiunzi cha nadharia, kwa hatua hizo matumizi ya kiambishi katika lahaja husika yaliangaliwa kwa upana.

SURA YA TATU

MBINU ZA UKUSANYAJI DATA

3.1 Utangulizi

Sura hii ni mkusanyiko wa sura ndogo ndogo ikiwemo muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, watafitiwa wa utafiti, zana za kukusanyia data na mipaka ya utafiti yote haya yalifanyiwa kazi katika sura hii na kwa ufafanuzi.

3.2 Muundo wa Utafiti

Utafiti uliwasilisha data kwa kutumia muundo wa tarakimu pia maelezo anuwai yalitumika kufafanua data hizo pale zilipohitajika. Hii ni kutaka kurahisisha uelewa kwa wahusika wanaojua kusoma hisabati na wale wasiojua kusoma hisabati.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulikusanywa data katika kisiwa cha Pemba, Mashariki Kaskazini na Kusini mwa kisiwa hicho, haya ni maeneo ya miji mikongwe ambayo inaaminika kuwepo kwa wakaazi wa asili wa kisiwa hicho. Maeneo hayo ni pamoja na Kiutumaziwang'ombe, Micheweni, Wingwi, Kojani, Kangagani, Vitongoji, Muambe na Kiwani katika kisiwa cha Pemba, sehemu hizi zinatoshwa kupatikana data kulinganana mada kwani kuna lahaja ndogo ndogo zinazojitofautisha kila moja na nyingine, lahaja hizo ndizo kwa pamoja zinazojumuika na kuunda Kipemba hiki kinachojulikana sasa duniani kote.

3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti ni Wapemba ambao wanapatikana katika Kisiwa cha Pemba. Walengwa waliekwa katika makundi mawili ya (wanawake na wanaume) kama

yaliyokusudiwa kushirikishwa katika utafiti huu, makundi yaliyoonekana na kutafsiriwa kwa rika na hadhi mbili; ambazo ni:-

- i) Hadhi ya wasiosoma.
- ii) Hadhi ya waliosoma kidato cha III na IV.

3.5 Watafitiwa wa Utafiti/ Uteuzi wa Sampuli.

Dhana ya sampuli inahusu uhusiano uliopo kati ya walengwa wautafiti na watafitiwa wa utafiti (sampuli). Dhana hii hutumika kwa uteuzi bahatishi wa watafitiwa (Kothari,1990). Sampuli ni kundi dogo la watafitiwa ambalo hupatikana kwa kupitia mchakato unaoendana na utafiti kwa lengo la kupata data zitakazowakilishwa katika mada badala ya kuweka kundi kubwa la watafitiwa.

Naye Sorencen (2010) anasema sampuli ni sehemu ya watu/vitu kidogo ambavyo huwakilisha watu wengi. Sampuli lazima iwe kiwakilishi, kwa maana ya kwamba lazima iwe na sifa sawa na kundi linalowakilishwa (Thungu, ameshatajwa) hutumia uteuzi wa walengwa kwa njia ya ushirikishaji ilihali kila kundi tafitiwa kati ya yale yaliyokusudiwa huwa na nafasi sawa ya kuteuliwa na kuwa na uwakilishi wa kundi lengwa.

Adam na Kamuzora (2008) wanasema sampuli ni watu, vitu au maeneo yaliyoteuliwa na mtafiti kwa niaba ya walengwa ili uchunguzi ufanywe kwa sharti la kupata taarifa sahihi juu ya jambo linalochunguzwa. Sampuli hupatikana kutokana na mbinu mbali mbali za usampulishaji. Usampulishaji nimchakato wa kuchagua idadi maalumu ya watu, vitu, kutoka kundi la walengwa kiasi kwamba idadi inayoteuliwa ina viashiria vya sifa zilizopo kwenye kundi kubwa la walengwa. Utafiti huu ulilenga

kuvigawanya na kuvipitia, kila kikundi kati ya vikundi viwili (wanawake na wanaume) kila kikundi kiliteuliwa watu (3) waliowakilisha watu 42, wanaotoka kwenye vijiji saba (7) ambavyo viliwakilisha kundi kubwa lisilojuulikana idadi rasmi.

3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu ulitumia mbinu mbali mbali ambazo zilisaidia kupatikana kwa data, ambazo zilitafsiriwa na kufafanuliwa kwa kutumia dhana elekezi za mbinu za ukusanyaji data kama zilivyoelekezwa na wataalamu mbali mbali wa isimu.

Kothari (1990) anafafanua dhana ya ukusanyaji data kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo ya utafiti. Mbinu za ukusanyaji data zilizohusika ni kama vile usaili, dodoso na uchunguzi makini. Kwa mujibu wa Vertanian (2011) data za msingi ni data ambazo zimekusanywa na mtafiti kufanya utafiti kwa kutumia mbinu kama hojaji, mahojiano, vikundi lengwa, uchunguzi au mbinu nyingine.

Kwa upande wa utafiti huu mbinu zilitumika kuwatafuta watafitiwa katika maeneo mbali mbali ni hizi zifuatazo:

3.6.1 Mbinu ya Usaili

Kwa mujibu wa Kothari (2009) usaili ni mbinu ya ukusanyaji data ambayo inahusisha uwasilishaji wa maswali ya mdomo na kujibiwa kwa njia ya mdomo, mara nyingi usaili hutumika kuwahoji wale watafitiwa wasiosoma. Katika utafiti huu mbinu hii ya ukusanyaji data ilitumika ili kupata data zilizotakiwa, mbinu hii

ilitumika kwa namna mbili tofauti, aina ya kwanza ni ile ya usaili kuwasaili wazee wasiosoma ana kwa ana, aina yapili ni ile ya usaili wa rununu kuwasaili wale ambao data zao hazikuwa wazi, njia hizi mbili zilisaidia sana kupatikana kwa data zilizohitajika katika utafiti huu.

3.6.2 Mbinu ya Dodoso

Kothari (2009) anasema dodoso ni mbinu ya ukusanyaji data ambapo mtafiti huandaa maswali katika karatasi na kuwataka watafitiwa wajibu. Dodoso katika utafiti huu lilitumika zaidi katika kuwahoji watu wanaojua kusoma na kuandika katika ukusanyaji wa data, ambapo mtafiti alitayarisha maswali na kuwataka watafitiwa wa utafiti kujibu kwa kupitia vikundi vya vijana katika shughuli za kijamii kama vile uvuvi, shuleni, viwanja vya michezo na wazee katika maeneo yao pia walipitiwa.

3.6.3 Mbinu ya Uchunguzi Makini

Ni njia ya siri inayowakutanisha mtafiti na mtafitiwa mahala pamoja, ambapo mtafiti hujibu maswali yanayohusiana na mada kwa siri ili kupata taarifa makini za utafiti. Mtafiti anaweza kutumia maswali kutoka katika maandishi aliyoyatayarisha awali ni muhimu kuwa na maandishi ambayo humsaidia kupata majibu yanayohusu mada iliyokusudiwa (Thungu, 2010). Mtafiti alikusanya data kwa siri katika vikundi vya mazungumzo ambapo alizihariri data zote na kugunndua ukweli wakiambishi kinavyotumika katika lahaja ya Kipemba, kwa kutumia mbinu hii mtafiti alipata muda wa kumuhoji kila mtafitiwa anaewakilisha kundi lililokusudiwa.

3.7 Zana za Utafiti

Hivi ni jumla ya vifaa vinavyosaidia kukusanya na kuhifadhi data. Vifaa mbali mbali vilitumika katika utafiti huu kwaajili ya kukusanya data za utafiti na kuweka kumbukumbu za utafiti, mfano wa vifaa hivyo nikama:

- i) Kalamu na Karatasi; ambazo zilitumika kwa kuweka kumbukumbu, hizi zilikuwa muhimu sana kwa vile ndizo zilizotumika katika ukusanyaji, uchanganuzina upangaji wa dodoso za data hizo.
- ii) Kompyuta mpakato (tarakilishi) ilitumika kwa kukusanya, kuhifadhi, kuchapisha kumbukumbu za data kutoka katika vyanzo mbali mbali.
- iii) Simu ya mkononi (rununu); ilitumika kwa mawasiliano kati ya mtafiti na watafitiwa, mtafiti na msimamizi na pia kunasia sauti kwa watafitiwa ili zitumike baadae.

3.8 Miiko ya Utafiti

Miiko/Maadili ni kaida zinazoelekeza tabia zetu katika mahusiano yetu ya kila siku (Mathooko na wenzake, 2007:uk,15). Katika utafiti, maadili ni uwajibikaji na uwelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote watakaotafitiwa, uwelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii ya binadamu. Kwa kuwa utafiti huu ulihusisha watu wa jamii mbalimbali na kwa sababu kila jamii ina sheria, taratibu, kanuni na utamaduniwake, mtafiti alilazimika kufata taratibu zilizomsaidia kuingia katika maeneo husika. Jambo jingine la kimaadili ambalo mtafiti alilizingatia ni kuwaomba washiriki kushiriki kwa hiari na kujitolea katika kutoa data. Vile vile mtafiti alizingatia usiri wakati wa kukusanya data kiasi kwamba hakuna mtu mwingine zaidi

ya mtafiti aliyejua chanzo cha data hizo na wala hakubainisha utambulisho wa mshiriki. Washiriki hawakutakiwa kuandika majinayao ili kulinda siri ya mtoa data. Kulingana na ahadi ambayo mtafiti alitoa kwa wahojiwa wake, data zote alizokusanya kutokanana rekodi ya usaili, daftari, notisi za uwandani na taarifa za hojaji mtafiti alizitunza kwa usiri mkubwa. Hii inaonyesha kwamba mtafiti alichukua hatua muhimu katika kuzingatia vipengele vyote vya maadili katika utafiti huu.

3.9 Hitimisho

Sura hii ilihusu data zilizokusanywa maeneo mbali mbali katika Kisiwa cha Pemba, pia utafiti ulihusisha mbinu, njia, zana mbali mbali za ukusanyaji data, walengwa na miiko ya utafiti ambayo ilizingatiwa kufanikisha utafiti huu.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA MATOKEO YA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Katika sura hii utafiti ulionesha data zilizokusanywa nakuchambuliwa, ambazo zimepatikana katika maeneo teule ya utafiti katika kisiwa cha Pemba. Aidha ndani ya sura hii kuna sura ndogo ndogo zilizofafanua data. Sura hizo nipamoja na sababu za kutumia Silabi katika lahaja ya Kipemba, vyanzo vya kiambishi “ka” na “ku”, makundi ya watafitiwa, utumiaji wa kiambishi “ka” na “ku”, mahusiano ya kiambishi na mofu zingine za kiambishi katika lahaja ya Kipemba, kuvuka mipaka kwa “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba ukilinganisha na kiambishi katika Kiswahili Sanifu, vile vile sura imezungumzia tofauti/mfanano wa kiambishi “ka” na “ku” katika maumbo na katika maana, hitimisho ambapo mfatano huu wa sura ndogo ndogo ndani yake ndio uliufanya sura hii uwe kwa muwala unaofahamika.

4.2 Sababu za Kutumia Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba

Sababu mbali mbali ambazo zilinukuliwa kutumia kiambishi katika maumbo lugha ya lahaja hii, ambazo zilitolewa na watafitiwa katika msamiati wa lugha, kudhihiri kwake kulitokana na madai mbali mbali yaliyotolewa na watafitiwa, jadweli lifuatalo lilitumika kufafanua sababu hizo.

Jadweli Na. 1: Likionesha Sababu za Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba

Na.	Watafitiwa	Asilimia	Sababu iliyotolewa
1	10	23.8	Sababu za kihistoria
2	7	16.66	Kulinda na kuzalisha msamiati
3	11	26.19	Haja ya mawasiliano na
4	14	33.33	Sababu ya utengano wa kijografia
Jumla	42	99.98	

Chanzo: Data za uwandani.

4.2.1 Sababu zilizochochea Kutumia Kiambishi Kihistoria

Kwa kuanzia na kuzifafanua sababu za kutumia kiambishi kutokanana historia ya watu, hii ilitokana na kuamua kutumia lahaja inayopatikana katika maeneo yao kutokanana kurithi kutoka kwa wazazi wao. Wakaazi wa maeneo mbali mbali Kisiwani Pemba wana vijilugha vya asili ambavyo huwajulisha na pia huwatofautisha nawenzao wanapoongea. Vijilugha hivyo vilijadiliwa na kuonekana kama vilivyoielezwa katika jadweli Na.1 hapo juu, ambapo watafitiwa 10 kati ya 42 ambao ni sawa na asilimia 23.80% ya watafitiwa wote walidai kuwa kiambishi huzuka kutokana na historia ya watu kutumia kijilugha chao. Watu hao walipoishi waliweza kutumia kijilugha chenye kiambishi katika kila kilahaja ambacho kwa pamoja kinaunda Lahaja ya Kipemba walisema.

Kielelezo Na.1. 1: Kikifafanua lahaja ilivyoundwa na kiambishi katika vijiji

mbali mbali Kutokana na historia.

Mwambe	Kangagani	Kojani	Kiwani	Kiuyu	M'weni	Wingwi	K 'sanifu
Kwanka	Ku-amka	Kwan`ka	Ku-amka	Kwan`ka	Ku-amka	Ku-amka	Ku-amka
Ku-omba	Ku-omba	Kwomba	Ku-omba	Kwomba	Kwomba	Ku-omba	Ku-omba

Chanzo: Data za uwandani.

Inasemekana kuwa maeneo haya ya utafiti ya Kisiwa cha Pemba ni miongoni mwa maeneo ya asili kihistoria, ni maeneo ya wenyeji wa kisiwa hicho na inaaminika kuwa vijilugha hivi ndio Kipemba cha asili kilichoongelewa hapo awali, kabla, wakati na baada ya Mkoloni wa mwanzo.

4.2.2 Sababu za Kutumia Kiambishi “ka” na “ku” kwa Kulinda Msamiati.

Sababu nyingine iliyotolewa na watafitiwa nikuwa walitumia kiambishi kutokana na kulinda na kuzalisha msamiati wa lahaja ya eneo lao. Watafitiwa 7 ambao ni sawa na asilimia 16.66% ya watafitiwa wote walitoa sababu nyingine ya kuzuka kiambishi, ilidaiwa kuwa ni kulinda na kuzalisha msamiati katika jamii zao, kila jamii kati ya zile zilizotafitiwa zilikuwa na msamiati, ziliung`ang`ania kutumia kutumia lugha tofautina na jamii nyingine, ambapo katika kila msamiati pia kulipatikana kiambishi, hata hivyo.

- i) Msamiati mwingi unaonekana kutumiwa kimazoea hasa katika maendeleo na upevu wa fonolojia ya lugha ya Kiswahili. Msamiati unaotumika katika lahaja ya Kipemba unaonekana kukomaa kwani tangu asili msamiati huo ulitumika hadi leo.

- ii) Msamiati uliopo katika Kiswahili Sanifu unaonekana kuwa na uhusiano wa karibu na lahaja hii, kila kijiji katika vijiji teule vilichangia baadhiya msamiati kwa kusanifishwa na kutumika katika Kiswahili Sanifu. Vijiji hivi kwapamoja vikiwemo vijiji vingine kutoka Pemba ambavyo havikutajwa katika utafiti, hufanya lahaja ya Kipemba, ambayo huchangia msamiati katika Kiswahili Sanifu .

Kielelezo Na.1. 2: Kikionesha Kiambishi “ka” na “ku” kutoka vijiji mbali mbali vilivyochangia kuzalisha Msamiati.

Mwambe	Kangagan	Kojani	Kiwani	Kiuyu	M’weni	Wingwi	K- sanifu
Ku-ji	Ku-ji	Ku-ji	Umekuja	Ku-ji	Ku-ji	Umekuja	Umekuja
Ku-vuni	Ku-vuni	Umevua	Umevuna	Kuvuni	Umevuna	Umevuna	Umevuna
Ka-limi	Kalimi	Halimi	Halimi	Kalimi	Kalimi	Halimi	Halimi
Ku-rudi	Hurudi	Kurudi	Kurudi	Kurudi	Umerudi	Umerudi	Umerudi
Ka-kipo	Hakipo	Kakipo	Hakipo	Kakipo	Hakipo	Hakipo	Hakipo
Ka-wapo	Kapo	Kayupo	Hayupo	Hayupo	Kawipo	Hayupo	Hayupo
Ka-lipo	Halipo	Halipo	Halipo	Kalipo	Kalipo	Halipo	Halipo

Chanzo: Data za uwandani.

4.2.3 Sababu zilizochochea Kutumia “ka” kutokana na Haja ya Mawasiliano

Sababu nyingine ambayo ilitolewa na watafitiwa kuwa ni miongoni mwa chanzo cha kutumia kiambishi ni pamoja na haja ya mawasiliano kati ya wanajamii hao pale wanapokutana, iwapo watafitiwa 11 kati yao ambao ni sawa na 26.19% walitoa sababu ya kutumia kiambishi kuwa ni haja ya mawasiliano, kwani kiambishi

huambatana na msamiati wa lugha hii inatokana na mahitaji ya wanajamii hao kila wanapokutana pamoja. Kwakuwa wanadamu wanahaja mbali mbali wanapokutana na watu wa utamaduni mmoja na hivyo lugha hiyo hutumika kama msingi mkuu wa kutatua haja hizo. Mfano walitakiwa wafanye maongezi mafupi wakaazi wa kijiji cha Muambe moja ya kijiji tafitiwa yalikuwa hivi:-

“Ka Hassani kanitumi kuwambili kwamba,
Msirejee kuja kuja kapa kwake,
Kwani kumakuja mara kwa mara,
Kumaleta uchoko”.

Kwa wakaazi wa kijiji cha Kangagani maongezi haya yanalikuwa kama hivi:-

“Ka Hassani kanitumi kuwambii kwamba,
Msirejee kuja hapa kwake,
Kwani mkirejela mara kwa mara,
Mnaleta uchon`ko”.

Kimsingi hii ni taarifa fupi tu ambayo iliagizwa kukomesha kitendo cha mikusanyiko ya vijana nyumbani pawatu kwani hutengeneza ufisadi, tunategemea maana ya kila kiambo cha kilahaja yanaweza kuwa.

Neno- Maana

Ka- Kaka

Kanitumi- Kanituma

Kuwambili- Niwambie

Msirejee- Msirejee

Kapa- Kukaa hapa

Kumakuja- Mnakuja

Kunaleta- Munaleta

Uchoko-Ugonvi

Utafiti ulionesha baadhi ya viambishi kutokanana haja ya mawasiliano, kila wanajamii hao walipowasilianana kiambishi“ka” na “ku”kikijitokeza katika mazongumzo yao, hii ndio ikaaminika kuwa kiambishi hiki ni moja ya kiambishi kinachopatikana kutokanana haja ya mawasiliano.

4.2.4 Sababu za Kuibuka Kiambishi kutokana na Umbali wa Kijografia

Baadhi ya watafitiwa waliofikia 14 sawa na 33.33% walidai kuwa umbali wa kijografia ni sababu inayochochea kuzuka kwa msamiati na kutofautiana kiambishi katika lahaja. Umbali uliopo baina ya kijiji cha Mwambe kwa mfano na maeneo mengine ya Pemba umesababisha watu wanaoishi Mwambe kutumia kiambishi na lahaja tofauti ukilinganisha na sehemu nyingine za Pemba.

Kielelezo Na.1.3: Kikieleza kuzuka kiambishi kutokana na umbali wa kijografia

Mwambe	Kangagani	Kojani	Kiwani	Kiuyu	M’weni	Wingwi	K- sanifu
Kapo	Kayupo	Kapo	Kayupo	Kayupo	Kayupo	Hayupo	Hayupo
Kaji	Kaji	Kaji	Kankuja	Kaji	Kaji	Kaja	Amekuja
Kuji	Kuji	Kuji	Umekuja	Kuji	Kuji	Umekuja	Umekuja
Kuvuni	Kuvuni	Umevua	Kuvuni	Kuvuni	Umevuna	Umevuna	Umevuna
Kalimi	Kalimi	Halimi	Halimi	Kalimi	Kalimi	Halimi	Halimi

Chanzo: Data za uwandani.

Msamiati mwingi ulionekana kutofautiana kulinganana umbali uliopo kati ya kijiji kimoja na kingine, msamiati hutofautiana kijiji hiki wakati huo huo hufanana na kijiji kingine katika msamiati ule ule. Utumiaji wa kiambishi upo wazi katika kielelezo hapo juu hatua moja moja hadi kufikia Kiswahili Sanifu. Sambamba na upatikanaji wa kiambishi ambacho kilionesha matumizi mbali mbali katika lahaja nyingi za

Pemba, pia kulikuwa na msamiati mwingi ambao ulitumika kutokanana mtengano wa kijografia katika maeneo ya Pemba.

Kielelezo Na.1.4: Kikionesha Msamiati ulivyozuka kutokana na Umbali wa Kijografia

M'weni	Kangagani	Kojani	Wingwi	Kiuyu	Mwambe	Kiwani	k-sanifu
Kwanka	Ku-amka	Kwan`ku	Ku-amka	Kwan`ka	Kudan`ka	Ku-amka	Ku-amka
Ku-omba	Ku-omba	Kudoea	Ku-lilia	Kwomba	Kwomba	Ku-omba	Ku-omba

Chanzo: Data za uwandani.

4.2.5 Muhtasari

Katika kujibu suali la utafiti huu, lililotaka sababu za kuzuka kiambishi katika lahaja, zimeonekana sababu ambazo watafitiwa wamebainisha, sababu hizo ni pamoja naumbali wa utengano kijografia, kutokana na kihistoria, kuzalisha msamiati na haja ya mawasiliano.

Mbali na sababu hizo, bado yako mambo madogo madogo ambayo hupelekea kuzuka kiambishi na msamiati. Sababu zenyewe ni kama vile matabaka ya kijamii, yanayotokana na elimu na dini.

Data hizi zilienda sambamba na Nadharia ya Maumbo. Nadharia hii inadai kuwa lugha huanza kwa kijineno kidogo sana katika jamii, kisha kupachikwa maumbo mbali mbaliya lugha na hupata uhai wa kimatumizi kijografia na kadiri muda unavyosonga mbele lugha hio hukua kimsamiati na hatimae lahaja mbali mbali huzuka.

4.3 Athari za Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba

Athari za kiambishi chochote huonekana katika msamiati, viambishi mbali mbali vya lugha pamoja na kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba hujitokeza katika msamiati na kuwa kiambishi njeo, nafsi, kiambishi tamati, mafumbo, kitarafa, kiambishi kinachojitokeza katika tungo zinazoonesha ukinzani na kivumishi

Jadweli Na. 2: Likionesha mgawanyiko wa Athari za kiambishi “ka” na “ku”

S/No	IDADI YA WATAFITIWA na JINSI ZAO NI: 42	ASILIMIYA	MAJIBU YALIYOTOLEWA
1	Wanawake- 3	16.66	Athari katika kiambishi njeo.
	Wanaume- 4		
2	Wanawake-2	11.90	Athari katika kiambishi nafsi.
	Wanaume- 3		
3	Wanawake- 2	11.90	Athari katika kiambishi tamati.
	Wanaume- 3		
4	Wanawake- 2	16.66	Athari katika mafumbo.
	Wanaume- 5		
5	Wanawake- 2	14.28	Athari katika vijiambo vya kitarafa.
	Wanaume- 4		
6	Wanawake - 2	14.28	Athari katika tungo ukinzani.
	Wanaume- 4		
7	Wanawake- 2	14.28	Athari katika kivumishi
	Wanaume- 4		
Jumla	42	99.96	

Chanzo: Data za uwandani.

Athari za Kiambishi “ka” na “ku” Njeo katika Lahaja ya Kipemba.

Tukianza na uwasilishaji na ufafanuzi wa matokeo ya data za utafiti kwa upande wa kiambishi njeo ambacho kilishughulikiwa. Jadweli Na.2 lililopo hapo juu lilifafanua zaidi jinsi majibu ya watafitiwa yalivyojitokeza kuchangia athari zakiambishi “ka” na “ku”. Jadweli hili lilifafanua kuwa majibu ya watafitiwa 7, ambao nisawa na asilimia 16.66% walidai kuwa kiambishi kinadhihiri kutokanana njeo. Ukweli ni kwamba kiambishi njeo hiki hutanguliwa na kiambishi nafsi kama zilivyo lahaja zingine za ulimwengu. Ufafanuzi zaidi unaonekana katika kielelezo kifuatacho hapa chini.

Kielelezo Na.2. 1: Kinafafanua athari za kiambishi kiwakilishi cha Njeo

Na.	Maneno	Na.	Maneno	Na.	Maneno
1	Ka-ku-shukuru	10	Ku-kuruka	19	Ha-ku-hangaika
2	Ka-ku-gharimu	11	Ha-ku-tunga	20	Pa-ku-saini
2	Ka-ku-tuma	12	A-ku-kumbuka	21	A-ka-kupenda
4	Ka-ku-kera	13	Wa-ka-salimia	22	Wa-ka-msifu
5	Ka-ku-kirimu	14	Ha-ku-faulu	23	Na-ku-kirimu
6	Ki-ka-potea	15	A-ku-penda	24	Wa-ku-laumu
7	Ha-ku-chagua	16	Ka-ku-tuma	25	Ka-ka-sirika
8	Ha-ku-mkera	17	Wa-ku-juwa	26	Ka-ku-fahamu
9	Ka-ku-korea	18	Wa-ku-amini	27	Ha-ku-niona

Chanzo: Data za uwandani.

Kielelezo Na.2.1 kilionesha idadi yawatafitiwa walioidai kuwa kiambishi hujitokeza katika njeo, ikiwa jumla ya majibuya watu 7 sawa na asilimia 16.66% ya watafiwa wote yalijibu kuwa kudhihiri kwakiambishi “ka” na “ku” hutokana na njeo.

Athari za Kiambishi “ka” na “ku” Kiwakilishi Nafsi katika Lahaja ya Kipemba.

Sambamba na hayo, utafiti pia ulibaini kiambishi katika kiwakilishi nafsi, iwapo watafitiwa 5 kati yao ambao ni sawa na asilimia 11.90% walijibu kuwa kiambishi hujitokeza katika nafsi ndani ya lahaja hii, kielelezo kifuatacho kilifafanua zaidi.

Kielelezo Na.2. 2: Kinafafanua kiambishi “ka” na “ku” kiwakilishi cha Nafsi.

Neno	Kiambishi nafsi	Neno	Kiambishi nafsi
Ka-limeni	II- wingi	Ku-tulii	I- umoja
Ka-toroka	III- umoja	Ku-kasiriki	II- umoja
Ka-yupo	III- umoja	Ku-dadisi	II- umoja
Ka-kutuma	III- umoja	Ku-jii	II- umoja
Ka-fa	III- umoja	Ku-umii	II- umoja
Ka-muuku	II- wingi	Ku-filiwi	II- umoja
Ka-nuka	III- umoja	Ku-tawali	II- umoja
Ka- wajaamua	III- wingi	Ku-fuati	II- umoja
Ka-zaliwa	III- umoja	Ku-salii	II- umoja
Ka-jaaliwa	III- umoja	Ku-lazimiki	II- umoja
Ka-wajaaliwi	III- wingi	Ku-uki	II- umoja
Ka-toroka	III- umoja	Ku-po	II- umoja

Neno	Kiambishi nafsi	Neno	Kiambishi nafsi
Ka-jaaliwa	III- umoja	Ku-taki	II- umoja
Ka-wauka	III- wingi	Ku-kereki	II- umoja
Ka-iba	III- umoja	Ku-chamii	II- umoja
Ka-wafuu	III- wingi	Ku-po	II- umoja
Ka-itwae	II- umoja	Ku-jaja	II- umoja

Chanzo: Data za uwandani.

Kiambishi kiwakilishi nafsi maranyingi hujitokeza katika kiwakilishi nafsi ya pili umoja/wingi nanafsi yatatu umoja/wingi. Kiambishi “ka” na “ku” kiwakilishi nafsi katika lahaja hii huwa nanafasi kubwa katika kundi la nafsi ya pili na nafsi yatatu kama ilivyoelezwa hapo juu.

Athari za Kiambishi “ka” na “ku” Tamati katika Lahaja ya Kipemba

Vile vile kiambishi hujitokeza katika utamatishaji wa maneno, baadhi ya msamiati haueleweki maana yake ila hufunguka maana yake kwa kuekwa kiambishi mwishoni. Hili lilielezwa na utafiti kwa upana, iwapo majibu ya watafitiwa 5 sawa na asilimia 11.90 % ya watafitiwa wote yalinukuliwa na kuonesha hivyo, mara nyingi kiambishi hiki huja kwa lengo la kukamilisha maana ya neno kama ilivyoelezwa maeneo mbali mbali ya utafiti huu.

Tukiangalia kwa makini misamiati ya hapo juu tutaona kuwa kiambishi “ka” na “ku” kinajitokeza mwishoni mwa kila msamiati kukamilisha maana, hali ambapo kiambishi hiki huja kwa kazi hii muhimu, kwani kabla ya kuekwa kiambishi hakuna msamiati wowote ambao ulieleweka. Kwamfano viambajengo -wakuali-, walizi-, shu-, kashapi- yote hayakueleweka.

Lakini baada ya kuekwa kiambishi tamati maana fiche hiyo ilieleweka kama-wakuali-ka, walizi-ka, shu-ka, kashapi-ka.n.k.

4.3.1 Athari za Mtumizi ya Kiambishi “ku” katika Mafumbo

Vile vile uchunguzi ulionesha kuwa baadhi ya viambishi hujitokeza katika mafumbo, kwani majibu ya watafitiwa washiriki 7 yalitolewa, ambayo ni sawa na asilimia 16.66% yote yalithibitisha matumizi hayo. Wakaazi wa maeneo haya walitumia mafumbo pale ambapo walitaka kueka ujumbe fiche juu ya jambo fulani walilotaka litendeke au lisitendeke. Mfano:-

Kusudi haiambiwa pole. hii ni kwa mtu aliekatazwa jambo ila alitenda na akapata hasara.

Umoja ukulani. Kutoa sadaka/ hongo kwa kutaka kufanikisha jambo.

Kufa n`kufaana Kitilia maanani kusaidiana.

4.3.2 Matumizi ya Kiambishi “ka” katika Mafumbo

Kawia ufike -hii ni kwa mtu aliekatazwa kufanya jambo kwa pupa. nk.

Sambamba na hayo kiambishi “ka na ku” kilionekana kikitumika kama **silabi/mofutu** ambayo huambatishwa na silabi nyingine na kuunda msamiati; miongoni mwa maneno hayo nipamojanakiambo (kitarafa) cha lahaja hii. Kiimbo sauti hiki huitwa kiambo kwani hutokea tofauti kimatamshi kati ya kijiji (kiambo) kimoja na kingine. Watafitiwa 6 pekee sawa na asilimia 14.28% walitoa majibuna kuonesha kuwa kiimbo sauti kinabainika kitarafa. Kiimbo hiki kinajitokeza mara kwa mara kutokananahisi za kilunga.

- i) Mara nyingine hutumika kuibua mshangao.
- ii) Mara nyingine hutumika kuwakiliha swali.

Kielelezo Na.2. 3: Kikionesha silabi “ka” kiwakilishi mshangao.

Na.	Maneno mshangao	Watumiaji wa kiambo/kitarafa	Maana katika K’ sanifu
1	Kamwe!	Ki-kiwani	Kimshangao
2	Aka!	Kivitongoji/M’ng’ombe	Kimshangao
3	Kaah!	Ki-kiwani/Ki-wingwi	Kimshangao
4	Akaa!	Ki-m’weni/ Ki-kiuyu	Kimshangao
5	Kaa!	Ki-kangagani/Ki-kojani	Kimshangao

Kielelezo Na.2.4:Kikionesha silabi “ku” kiambo.

Na.	Maneno mshangao	Watumiaji wake	Maana katika Kiswahili sanifu
1	Kumbe!	Ki-kiwani/Ki-wingwi	Kimshangao
2	Kun’kuja!	Ki-kiwani/Ki-wingwi	Kimshangao
3	Kuumbee!	Ki-m’weni/Ki-kojani	Kimshangao
4	Kumbee!	Ki-kangagani	Kimshangao
5	Kuwapo!	Ki-muambe	Kimshangao
6	Kupo!	Ki-maziwang’ombe	Kimshangao
7	Kuji!	Ki-kojani	Kimshangao
8	Kuumbe!	Ki-micheweni	Kimshangao

Chanzo: Data za Uwandani.

Kama tulivyoeleza hapoawali kuwa kipaza sauti/kiimbo hiki hujitokeza mara kwa mara kutokanana hisi za kilugha, sauti tofauti hupatikana kutokanana mparazo wa hewa wakati wa utamkaji wa viimbo hivi, kwa sauti ya juu au sauti ya chini yote ni

matumiza ya kiambo, ambapo hutegemea kiimbo na haja ya wanajamii, maranyingine hutumika kuwakilisha swali pale inapobidi kuuliza, mara nyingine hutumika kuibua mshangao. Kiambo “ka” na “ku” kikiambatishwa na silabi nyingine huwakilisha swali, utafiti ulibaini kuwa watumiaji wa lahaja hii huunda swali pale ambapo “ka” au “ku” itaambatishwa na silabi nyingine inayoweza kuunda neno linalofahamika na jamii hiyo.

Kielelezo Na.2. 5: Kikionesha silabi “ka” ikiwakilisha swali kwa kuambatishwa na mofu.

Na.	Neno swali	Na.	Neno swali
1	Kamwe?	4	Aka?
2	Kah?	5	Akaa?
3	Kaa?	6	Kafuu?

Chanzo: Data za uwandani.

Kielelezo Na.2. 6: Kikionesha Silabi “ku” ikiwakilisha swali kwa kuambatishwa na mofu.

Na.	Neno swali	Na.	Neno swali
1	Kumbe?	7	Kuwapo?
4	Kumbee?	10	Kupo?

Chanzo: Data za uwandani.

4.4 Matumizi ya Silabi “ka” na “ku” katika Tungo Masharti

Baadhi ya watafitiwa walidai kuwa silabi hudhihirika katika lahaja ya Kipemba nakuzalisha tungo masharti. Tungo hizi zilitumiwa zaidi na watafitiwa watuwazima

wenye wastani wa miaka 45 -70 nakuendelea, iwapo watafitiwa6 walichangia majibu kati yao ambayo nisawa na asilimia 14.28% ya watafitiwa wote, mara nyingi wazo fulani kutokeakwake ni lazima kutendeke kwa jambo jingine la awali. Kwa muhtasari kabisa tungo hizi zilikuwa kama:-

Akutukanaye hakuchagulii tusi.

Akulaumuye akupenda.

Akufaaye kwa dhiki ndiye wako rafiki.

Akufukuzaye hakuambii toka..

Udugu nikufaana udugu sikufanana.

Ukuu kuu wa kamba si upya wa ukambaa.

Kutangulia sikufika.

Kutembeya nikusoma.

Watafitiwa walidai pia silabi hii hutumika kama kihusishi, kwa mchango wao watafitiwa 6waliojibusawa na asilimia 14.28% ya maswali ya utafiti wote. Walidai kuwa silabi hujitokeza katika maumbolugha na kuibua dhana ya uhusishi. Kwa uchunguzi wa utafiti huu uligundua kuwa kuna kiwakilishi nafsi ambacho hudokeza uhusika wa jambo.

Kielelezo Na.2.7: Kikionesha Kiambishi “ka” na “ku” kiwakilishi cha Kihusishi.

Na.	Maneno	Na.	Maneno	Na.	Maneno
1	Ka-ku-shukuru	10	Ku-ka-tibuka	19	Ha-ku-hangaika
2	Ka-ku-gharimu	11	Ka-ku-tuma	20	Pa-ku-saini
2	Ka-ku-tuma	12	Ka-ku-pa	21	A-ka-kupenda
4	Ka-ku-kera	13	Ka-ku-salimia	22	Wa-ka-msifu
5	Ka-ku-kirimu	14	Ha-ku-faulu	23	na-ku-kirimu
6	Ki-ka-potea	15	Ku-ka-pendeza	24	Wa-ku-lamu
7	Ha-ku-chagua	16	Ka-ku-tuma	25	Twa-ku-laumu
8	Ha-ku-mkera	17	Wa-ku-juwa	26	Ka-ku-fahamu
9	Ka-ku-korea	18	Wa-ku-kagua	27	Ha-ku-niona

Chanzo: Data za uwandani.

4.5 Makundi ya Watumiaji wa Kiambishi/Silabi “ka” na “ku”

Watumiaji wa kiambishi katika lahaja ya Kipemba hupatikana kulinganana haja ya mazungumzo yao. Makundi hayo huzungumza lahaja hii kwa upeo mkubwa, katika utafiti huu makundi hayo yaliteuliwa kulinganana rika na jinsi zao. Kama yalivyogusiwa katika 4.1 hapo juu, ambapo jumla ya maswali 79 yaliulizwa, katika utafiti na majibu yalipatikana kama yalivyotakiwa kwa watafitiwa hao, nao waligawanyika hivi kuonesha ushirikiwao.

Kielelezo Na.2.8: Kikionesha Mgawanyiko wa Majibu ya Watafitiwa

JINSI ZAO	KUNDI LENGWA	IDADI N=79	ASILIMIA %	NDIYO KUNA VIAMBISHI	HAKUNA VIAMBISHI	SIJUI - V^MBISHI
W^Wake	Vijana	6	14.28	√		
	Vijana	7	16.66		√	
	Wazee	2	2.53			√
W^Ume	Vijana	10	23.80	√		
	Wazee	10	12.65		√	
	Vijana	7	16.66			√
	Jumla	42	99.98			

Chanzo: Data za uwandani.

Aidha majibu haya yalikuwa yakipatikana maeneo mbali mbali ya kazi, kama uvuvi, biashara, kilimo na elimu. Maeneo muhimu ya wakazi wa kisiwa kidogo cha Kojani na Kiuyu Maziwang'ombe ni bandarini ambako watu hukaa kusubiri biashara ya samaki huku wakiendeleza shughuli zao nyingine za maisha kama vile ushonaji wa kofia, usukaji wa kamba nk. Maeneo kama vile Wingwi, Kangagani na maeneo mengine data zilipatikana katika sehemu za biashara kama vile sokoni, ambapo watu wengi hukusanyika kwa kufanya kazi mchana kutwa kwa ajili ya kujikimu kimaisha. Sambamba na hayo watafitiwa walifatwa maeneo ya mbali hata wale waliokuwa shambani ambapo wengi wa wakazi wa kisiwa cha Pemba hudumu huko kutwa kwa shughuli zao za maisha ya kila siku. Ama data zilizochukuliwa kutoka kwa wanafunzi hizi tunaelewa yakuwa zilipatikana kwa urahisi shuleni. Makundi yote

mawili; wanafunzi wa kike nawakiume yalishirikishwa kwa wakati mmoja. Mwisho ni kwa akinamama ambao walifuatwa na mtafiti katika makaazi yao, kwani Wapemba wa jinsi ya kike nemiiko kwao kwenda kununua bidhaa sokoni kikawaida.

4.5.1 Jinsi za Watafitiwa

Kielelezo Na.2.9: Kikionesha Idadi ya Washiriki na Jinsi zao.

Washiriki	Idadi yao	Umri wao	Asilimia
Wanaume	27	18- 83	64.28%
Wanawake	15	18- 79	35.71%
Jumla	42	-	100%

Chanzo: Data za uwandani.

Kielelezo hiki kinafafanua kiasi gani washirikiwa utafiti huu walivyoshirikishwa juu ya suala zima la matumizi ya kiambishikatika lahaja ya Kipemba. Jumla ya watafitiwa 27 walikuwa ni wanaume na ndio ambao waliifanya idadi hii kuwa sawa na asilimia 64.28%. Iwapo idadi hii ilijumuisha watafitiwa wasomi na wale wasio wasomi kama walivyoelezwa katika 4.1 hapo juu. 15 ya watafitiwa walikuwa wanawake nao walishirikishwa kwa kiasi ambacho mchango wao ulionekana kwa asilimia 35.71%, ambayo ilipatikana kwa kujumuisha watafitiwa kiasi 15ya watafitiwa wote.

Kwa ujumla watafitiwa wote hawa walikuwa na fursa sawa ya kuingizwa katika utafiti kwakuulizwa maswali kulinganana matayarisho ya utafiti huu, kwahivyo majibu ya makundi haya mawili yalionesha kuwa matumizi ya kiambishi husika kama kilivyoelezwa yanapatikana.

4.5.2 Muhtasari

Katika kujibu swali hili lililotaka kujua migawanyiko ya athari za kiambishi katika lahaja ya Kipemba, data zilifafanua athari zilizoelezwa na watafitiwa kuwa ni pamoja na njeo, kiambishi nafsi, kiambishi tamati, watumiaji wa kiambishi na jinsi zao.

4.6 Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika Nyanja mbali mbali za Lahaja hii

Mgawanyiko wa matumizi ya kiambishi katika lahaja yalionekana katika maeneo mbali mbali ambayo watafitiwa walieleza kwa umakini kabisa, kila kundi kati yao lilitoa mchango wa kimatumizi ya kiambishi katika lahaja ya Kipemba, maeneo ya matumizi hayo nipamoja na:-

4.6.1 Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” kutokana na Historia

- (i) Wakaazi wa Pemba wapo katika eneo dogo la kisiwa hali ambayo inawawezesha kukutana pamoja, hata hivyo kila mtu huwa anatoka kwao na lahaja yake fasaha inayoongelewa katika maeneo yao. Lahaja hii mara nyingi huathiriwa na mambo yanayohusu mila na itikadi za wanajamii hao, kwa mfano lahaja hizi mbili hutofautiana kulingana na itikadi za jamii husika: Mfano Kiuyu maziwan`gombe na Kimuambe.

- (i) Kiuyu maziwan`gombe

Kunambili ke Kombo kaniikili agizo, kaja umbi umbi

lakini kafika kakuna ndudu ya mtu kwakwe

hebunambila yanielee nikweli au nasahau ?.

Kwa wakaazi wa Maziwang'ombe kiambishi hiki hutamkwa kikiwa na shada kali na mpumuo mbali na kazi za kiambishi kilivyotajwa 4.1 katika utafiti huu.

- i) /ku/ hutamkwa /k^h/+ mpumuo , shada kali ~ ♪.
- ii) /ka/ hutamkwa /k^h/+mpumuo, shada kali ~ ♪.
- iii) /ke/ hutamkwa/k^h/+ mpumuo, shada kali ~ ♪.

Matumizi ya viambishi hivi viliathiri mawasiliano yao, hata hivyo watu hufahamiana bila shida katika kupokea ujumbe kati yao. Ambapo kwa mtu wa mazingira mengine ingekua uzito wa kuyatambua mazungumzo hayo yakizungumzwa mbele yake, hasa iwapo ni siku ya kwanza kusikia maneno hayo. Maneno haya yangalikuwa na maana kama hivi:-

Neno-	Maana.
Kunambili-	umeniambia
ke Kombo-	kaka Kombo
kaniikili agizo-	kaniikea agizo
kaja umbi umbi-	nikaja haraka haraka
lakini kafika kakuna-	lakini hafika hakuna
ndudu ya mtu kwakwe-	mtuhata mmoja kwake
hebunambila yanielee-	hebu nifahamisha
n`kweli `o`nnasahau ? -	nikweli au nimesahau?

(ii) Kimuambe.

Kunambili ka Kombo kaniikili agizo, kaja chwe
lakini kafika hakuna
ndudu ya mtu kwakwe

hebu namb`iya nielee

nikweli au nasahau ?.

Utofauti wa baadhi ya lafudhi hizi zilizopo katika utanzu huu wa lahaja hizi mbili haukuathiri maana ya utungo huo kwa wakaazi wa maeneo teule yaliyobakia, wote wangalimuelewa mzungumzaji anapotoka na anamaana gani juu ya kile alichokisema.

4.6.2 Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika Kuendeleza Mila

Wengi wa watafitiwa walikiri kuwepo kwa kiambishi ambacho kilidaiwa kutumika katika shughuli mbali mbali za maisha ya kilasiku. Miongoni mwa matumizi ya kiambishi ni pamoja na shughuli za kujenga mila zao. Mila iliohojiwa na kubainishwa na utafiti huu ni ile inayohusu mafunzo ya mtoto wa kike; yaani mwari, juu ya kuishi na mume katika ndoa kuwatendea wema wazazi wa mume wake yaani (wakwe zake). Mfano msamiati kadhaa ulitumika katika muktadha wamafunzo ya bibi arusi.

Ku-injika – kueka makazi mazuri wakati wa kula bwana.

U-kungwi- mkufunzi wa mwari/bibi arusi.

Ku-toka- matembezi ya mwari/arusi siku ya saba (7).

Ku-timbwa- mafunzo ya mwali/biarusi kwaajili ya mume.

Ku-kungika- pikika katika maafunzo ndani ya ndoa.

4.6.3 Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika Mambo ya Itikadi

Wananchi wa kisiwa cha Pemba katika kijiji cha Micheweni wana itikadi sahihi wanazoziamini katika maisha hasa kuhusu suala la malezi ya watoto wao, katika

nyanja ya utamaduni wao, walidhibiti kizazi chao. Utafiti ulibaini kuwa wakaazi wa Micheweni walizingatia sana malezi ya pamoja kwa watoto wao, walitaka mafunzo yao yarithiwe na kizazi chao. Miungoni mwa itikadi za wanajamii hawa ni kuwa hawaruhusu vijanawalio nje ya ndoa kuhudhuria sherehe zinazohusu taarifa za watu wazima, watoto walitengwa na maneno kama vile; mapenzi, ushoga, uchumba, talaka, wivu, umbea na kadhalika, wakiamini kuwa mambo hayo yote huchangia kuamsha hisia za mapenzi kwa watoto wakiwa wadogo shuleni. Kinyume chake watoto waliruhusiwa michezo inayolingana na shughuli zao kama; kifichoficho, foliti, fori, gware, taro, pia, na kadhalika. Mengi ya maneno ya michezo hii yalitumia kiambisi katika kudumu kwake na kuendeleza itikadi zao.mfano:-

Viambishi katika mchezo wa Kinyuli.

Kinyuli nyulika,
 Mwanangwa mwanajumbe,
 Ka-vaa nguo mbili,
 Ya tatu ka-jibandika,
 Kakasi na ulimbo,
 Aliyejuu naushe.

Viambishi katika mchezowa taro

Moja n-ku-roja
 Tumbili ka-vaa koja
 Enenda akijikongoja,
 Kwa mguu mmoja mmoja.

Aidha waliwachagua watoto wao nguo maalumu wasichana wao, wakiamini kuwa zinawadumisha katika hali ya utoto kimaumbile, hata kama wana umri mkubwa, nguo walizozichagua ni kanzu ya umbo mfuto (kamili), kanga ya kujifunga muwaa kifuani kwa kujibana ili maumbile yao yasisujudu haraka, waliamini maumbile hayo yakiachiwa mtoto angali tamani na kuanza mapenzi haraka.

Wapemba pia wanaweza kutumia kiambishi hiki katika maongezi kama ni utambulisho, utambulisho wao wa kimaeneo ambao unaweza kumsaidia msikilizaji wowote mjua lugha kumbaini msemaji pahala anapotoka. Hii ilitokanana kukomaa kwa lahaja hii katika wasemaji wake.

4.6.4 Muhtasari

Katika kujibu swali hili lililotaka kujua chanzo cha utokeaji wa kiambishi katika lahaja ya Kipemba, sura ilifafanua chanzo cha kiambishi katika maeneo mbali mbali ya matumizi ya lugha kama yalivyoelezwa na watafitiwa wahusika kwamba ni utumiaji wa Kihistoria, Mila na Itikadi za wanajamii.

4.7 Mahusiano ya Silabi “ka/ku” na Mofu zingine za Lugha

Kama tulivyoona hapo awali “ka” na “ku” hufanya kazi kama silabi tu katika Lahaja ya Kipemba, kama tunavyoelewa kiambishi/silabi ni kipande kidogo ambacho huambatishwa katika maneno, hudhihiri kabla nabaada ya mzizi wa neno, utokeaji wake huwa awali ya neno au wakati mwingine hutanguliwa na mofu zingine za uambikwaji kuchimbua dhana za kiisimu zilizomo ndani ya neno hilo. Tukiangalia tutabaini ya kuwa kuna mahusiano ya karibu kati ya Silabi “ka/ku” na mofu zingine za lugha, maelezo haya yanaweza kuthibitisha kama ifuatavyo:-

4.7.1 Mahusiano ya Silabi “ka” na Mofu zingine za Mzizi Mwanzoni

-ka +di	/kadi/
- ka +pa	/kapa/
-ka +ta/kata/	

Mahusiano ya Silabi “ka” na Mofu Zingine za Mzizi Mwishoni

-du +ka	/duka/
- pa +ka	/paka/
- sho+ka	/shoka/
- shu+ka	/shuka/
- So +ka	/soka/
-ta + ka	/taka/
-te +ka	/teka/
-tu + ka	/tuka/

Kama tunavyoelewa makusano haya ya Silabi “ka” na “ku” katika mzizi wa neno huwa ndivyo yanavyojitokeza katika mofu mbali mbali za lugha katika kuunda msamiati. Maelezo ya Silabi yalihusu uambatishwaji wake mwanzoni au mwishoni na dhima yake ni kutoa dhana ya neno kama invyodhihiri hapa juu.

Mahusiano ya Silabi “ku” na Mofu Zingine za Mzizi Mwanzoni

- ku +dra	/kudra/
-ku + ti	/kuti/
-ku +ra	/kura/

Mahusiano ya Silabi “ku” na mofu zingine za mzizi mwishoni

-pe + ku	/peku/
-suma+ ku	/sumaku/
-tumba+ ku	/tumbaku/
-shau+ ku	/shauku/

Kazi ya lugha yoyote ni kutumia mofu hizi ambazo utokeaji wake hutangulia au hutanguliwa na silabi zingine katika mzizina kuunda neno. Tukichunguza mofu zilizojitokeza hapo juu zote takribanini mafu huru, kazi yake huunganana Silabi nyingine kukamilisha neno (jina au kitenzi), hivyo ndipo kwa pamoja huibua dhana ya neno hilo. Hii ni kama kazi inayotekelezwa na mofu mbali mbali za lugha ya Kiswahili Sanifu sambamba na lahaja ya Kipemba .

4.7.2 Mahusiano ya Kiambishi “ka/ku” na Mofu Zingine Katika Kuibua

Dhana

Ka +niti	/ka/	- mofimu awali nafsi ya tatu, mtenda. -mofimu awali njeo ya wakati timilifu.
Ka+oo	/ ka/	- mofimu awali nafsi ya tatu, mtenda. -mofimu awali njeo ya wakati timilifu.
Ka+po	/ka/	- mofimu awali nafsi ya tatu, mtenda. -mofimu awali njeo ya wakati uliopo.
Ku+lia	/ku/	- mofimu awali nafsi ya pili, mtendwa. -mofimu awali njeo ya wakati timilifu.
A+ku+saka	/ku/	-mofimu awali njeo ya wakati uliopo.

Kila kiambishi katika hivi kilifanya kazi ya kuibua dhana fiche ambayo hujulikana kiisimu ndani ya maumbo lugha, dhana hizi zilikuwa na kazi mbali mbali kama vile; kudokeza wakati, nafsi, umoja na wingi. Mofu hizi wakati mwingine zikitumika katika nafsi hudokeza dhana ya umoja na wingi katika maumbo ya maneno.

4.7.3 Mahusiano katika sifa za kuambatishwa na mzizi

Kama tulivyoeleza awali kuwa moja kati ya sifa ya kiambishi ni kuegemezwa au kuambatishwa na mzizi wa neno ili kukamilisha neno hilo liweze kuleta maana/dhana za neno hilo baada ya kuambishwa.

Kielelezo Na.2.10: Kikionesha Uhusiano wa “ka/ku” na Mofu zingine katika

Sifa zao

Mofu	Mzizi	Neno	Dhana katika kiambihi
Ka	fu	Kafu	Kiambishi awali, nafsi ya tatu, umoja, wakati
Ka	tukuu	Katukuu	Kiambishi awali, nafsi ya tatu, umoja, wakati timilifu
Ka	ta	Kata	Kiambishi awali, nafsi ya tatu, umoja, wakati timilifu
Ka	ga	Kataga	Kiambishi awali, nafsi ya tatu, umoja, wakati timilifu
Ka	ka/ke/o	Kaka/kake/ ka-o	Kiambishi awali, nafsi ya tatu, umoja, wakati timilifu
Ka	tunguka	Katunguka	Kiambishi awali, nafsi ya tatu, umoja, wakati timilifu
Ku	po	Kupo	Kiambishi awali, nafsi ya pili, umoja, wakati uliopo

Mofu	Mzizi	Neno	Dhana katika kiambihi
Ku	wapo	Kuwapo	Kiambishi awali, nafsi ya pili, umoja, wakati uliopo
Ku	ji	Kuji	Kiambishi awali, nafsi ya pili, umoja, wakati ujao
Ku	twambili	Kutwambii	Kiambishi awali, nafsi ya pili, umoja, wakati uliopita
Ku	chi	Kuchi	Kiambishi awali, nafsi ya pili, umoja, wakati uliopita
Ku	vii	Kuvii	Kiambishi awali, nafsi ya pili, umoja, wakati uliopita

Chanzo: Data za uwandani.

Ukitoa kiambishi/mofu ya tano katika jadwali hili ambacho ni - /+ mzizi (neutral) inaonekana kuna tofauti kidogo, lakini ukiangalia kwa undani utabaini kuwa mofu zote zimeegemezwa katika mzizi au mofu nyingine na kuunda neno, kwa mfano mofu/kiambishi kutoka kolamu ya kwanza ya viambishi katika jadwali hili kinaungana na kolamu ya pili ya mofu/mzizi wa neno ambalo huambatishwa na hatimae kupata neno kamili kama ilivyo katika viambishi vya lugha nyingine. Na kwa upande wa maana, maana mbali mbali zilizofichika ndani ya mofu za lugha hudhihirishwa na viambishi vya lahaja iwapo vitafanyiwa kazi kiisimu. Kwa kawaida neno huundwa na mofu zilizoambikwa, wakatimwingine neno huundwa na mofu za mzizi, ambazo ndani yake hujitokeza mofimu zinazoelezea maana ya vijenzi hivyo kama zinavyoonekana katika jadwali.

4.7.4 Muhtasari

Katika kujibu swali hili lililotaka kujua uhusiano wa kiambishi “ka/ku” na mofu zingine katika lahaja ya Kipemba, data zilionesha uhusiano mbali mbali wa viambishi vya lugha kama yalivyoielezwa na watafitiwa wahusika. Aidha uhusiano huu ulikuwa katika kuunda msamiati, katika kuunda dhanana, sifa zao, katika kuisaidia lugha.

4.8 Kuvuka mipaka kwa kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja hii

Kiambishi “ka” na “ku” kinaonekana kupanda daraja ya matumizi kikilinganishwa na viambishi vya Kiswahili Sanifu. Kiambishi “ka” na “ku” hufanya kazi zaidi ya moja, huwakilisha wakati tofauti iwapo katika desturi ya lugha Sanifu kuna kiwakilishi maalumu kimoja cha wakati. Utafiti huu ulikuwa na lengo lakuchunguza uhusiano wa midhihiriko na matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba. Midhihiriko hii pia ilionesha tofauti kidogo kati ya kiambishi husika na vile vya Kiswahili Sanifu. Miongoni mwa tofauti hizo nipamoja na:-

Viambishi njeo vya lugha Sanifu Viambishi njeo vya lahaja ya Kipemba

(Huwa na mawanda finyu ya matumizi) (Huwa na mawanda mapana ya matumizi)

na -wakatiuliopo- analima	/ka/kanalima - wakati uliopo
Me -wakati timilifu- amefika	/ka/ kafika - wakati timilifu
Li -wakati uliopita – alinipa	/ka/kanipi - wakati uliopita
Ta -wakati ujao – atalima	/ka/katalima - wakati ujao
Hu - wakatimazoeya- husoma	/ku/ kusoma -wakati mazoeya
Ki - wakati masharti- ukilima utavuna	/ka/talima katavuna-wakati ujao masharti

Kuvuka mipaka kwa kiambishi “ka” na “ku” kilibainika katika njeo ya Kiswahili Sanifu na zile njeo za lahaja ya Kipemba. Ambapo kiambishi “ka” na “ku” kiliwakilisha njeo zote sita za wakati zilizoko katika lugha ya Kiswahili sanifu. Tukiangalia hapo juu katika maelezo tunaona kila kiambishi cha Kiswahili Sanifu kiliwakilisha wakati mahasusi ambao ni tofautina kiambishi kingine. Lakini kiambishi “ka” katika lahaja ya Kipemba kimewakilisha nyakati nyingi isipokuwa wakati mazoeza ambao umewakilishwa na kiambishi “ku”.

Vile vile kuvuka mipaka katika kutambulisha nafsi mbali mbali, kiambishi “ka” na “ku” hutofautiana na viambishi vingine kwani kundi moja la viambishi kati yao huchukua nafasi kubwa ya kimatumizi zaidi ya kundi jingine, ambalo lina nafasi finyu. Kiambishi nafsi cha lahaja ya Kipemba hutangaa nakuwakilisha nafasi zote kwa kupitia “ka” na “ku”.

Viambishi vya Kiswahili Sanifu

Viambishi vya lahaja ya Kipemba

(Huwa na mawanda finyu ya matumizi)
matumizi)

(Huwa na mawanda mapana ya

Tu+naimba-nafsi yakwanza wingi
umoja/wingi

/ku+naimba-nafsi ya pili

A+nalima-nafsi yatatu umoja

/ka+nalima -nafsi tatu umoja

Wa+nacheza-nafsi yatatu wingi

/ka+nacheza -nafsi yatatu wingi

Mu+lishinda -nafsi yapili wingi

/ku+lishinda -nafsi yapili wingi

U+lipika -nafsi yapili umoja

/ku+lipika -nafsi yapili umoja

4.8.1 Tofauti ya Maumbo Maneno ya Lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu

Maumbo maneno ya lahaja hii hutofautianana maumbo ya Kiswahili Sanifu; tukiangalia tutabaini kwamba maumbo haya yanatofautiana katika kuekwa/kutoekwa kiambishi kwenye mzizi wa neno, mara nyingine maumbo ya lahaja hutamkwa kisilabi tu, baadhi ya maneno ya lahaja ya Kipemba hutawaliwa sana na mkato; yaani hudondoshwa viambishi kadhaa ila hubaki na maana sawiya zinazotokana na neno hilo hilo katika lugha Sanifu.

Kielelezo Na.2. 11: Kikionesha Maumbo Maneno yalivyodondoshwa na Kuleta

Maana

Lahaja ya Kipemba		Lugha Sanifu	
Maumbo	Kiambishi zake	Maumbo	Kiambishi zake
Kapo	/ka-po/	Hayupo	/ha-yu-po/
Kaji	/ka-ji/	Amekuja	/a-me-ku-ja/
Kafu	/ka-fu/	Kafariki	/ka-fa-ri-ki/
Uka	/u-ka/	Ondoka	/o-ndo-ka/
Eka	/e-ka/	Weka	/we-ka/
Kucha	/ku+cha/	Kuchwa	/ku-chwa/
Kanambii	/ka-na-mbi-i/	Amenambia	/a-me-mbi-a/
Kaoo	/ka-o-o/	Ameowa	/a-me-o-wa/
Kaoni	/ka-o-ni/	Haoni	/ha-o-ni/
Kaowegwa	/ka-o-we-gwa/	Kaolewa	/ka-o-le-gwa/
Kasikili	/ka-si-ki-li/	Hasikii	/ha-si-ki-i/

Chanzo: Data za uwandani.

Tukizingatia jozi za maneno ya lahaja ya Kipemba mara nyingi zinaonekana pungufu kutokana na kudondoshwa idadi kadhaa ya kiambishi au kuekwa mbadala (kiambishi). Mfano

- Kapo- neno hili lina tofauti ya kudondoshwa kiambishi/ kabadala /ka/+po
asili ya neno hili ni
- Hayupo- neno hili lina idadi kubwa ya viambishi, kupachikwa vibadala
/ha/+yup+/o/
- Eka- neno hili lina idadi ndogo ya herufi, kutokana nakudondoshwa
kons/ir(w),katika lahaja ya Kipemba, lakini katika Kiswahili Sanifu
neni hili hutamkwa
- Weka- neno hili lina idadi kubwa ya viambishi, kwa kupachikwa kons-ir
(w), na kuwa kiambishi awali “we” (kons+ir) +ka, nk.

Vile vile katika minyambuliko yao maneno mengi ya Kiswahili Sanifu hufata kanuni za minyambuliko lakini baadhi ya nafsi katika lahaja ya Kipemba haziingii katika mizani ya unyambulishaji na hayawezi kujitegemea ila hukopa taswira kutoka Kiswahili Sanifu. Mfano:

- Ks .s aliimba- waliimbiana- muliimbashana- tuliimbana
- L .kp kaliimba- 0 liimbiana- kuliimbiani- kuliimbana
- Ks .s uliimba- uliimbiana- uliimbishana- uliimbana
- L .kp kuliimba- kuliimbiana- kuliimbishana- kuliimbana
- Ks .s waliimba- waliimbiana- waliimbishana- waliimbana
- L .kp waimbi- waimbiani- waimbishani- waimbani

Ks .s	tuliimba- tuliimbiana- tuliimbishana- tuliimbana
L .kp	tuimbi- tuimbiani- tuimbishani- tuimbani
Ks .s	muliimba- muliimbana- muliimbishana- muliimbana
L .kp	muimbi- muimbiani- muimbishani- muimbani

Maumbo haya ya lahaja ya Kipemba hayanautanganifu katika minyanbuliko, kwani baadhi ya minyambuliko yake imetumia maumbo mbali mbali ya Kiswahili Sanifu. Zaidi tukichunguza matumizi ya kiambishikatika maelezo haya tunaona kuwa hayakujitokeza maranyingi hasa katika

- nafsi ya III -wingi,
- nafsi ya II -wingi na
- nafsi ya II - umoja.

Ama katika nafsi ya tatu-umoja napili-umoja kiambishi kimechukua nafasi yake katika kuwakilisha nafsi. Zaidi ya hayo baadhi ya viambishi vilivyotumika katika unyambulishaji hukopwa kutoka katika lugha ya Kiswahili Sanifu.

Tofauti nyingine, viambishi vya aina moja katika lahaja ya Kipemba hufanya kazi zaidi, maumbo haya yanaweza kuwakilisha nafsi na wakati huo huo yanaweza kuwakilisha njeo. Bali katika Kiswahili sanifu kuna maumbo maalumu ya nafsi na maalumu ya njeo.mfano

Kiambishi Mahsusi cha nafsi.

NI	-kiambishi awali nafsi ya kwanza umoja.	Mimi ni -nasoma.
U	-kiambishi awali nafsi ya pili umoja.	Wewe u -nasoma.
WA	- kiambishi awali nafsi ya tatu wingi.	Wao wa -naandika
TU	- kiambishi awali nafsi ya kwanza wingi.	Sisi tu - naandika.
A	- kiambishi awali nafsi ya tatu umoja.	Yeye a - naanika.
MU	- kiambishi awali nafsi ya pili wingi.	Nyinyi mu -naandika.

Viambishi hivi vinavyounda kipashio-**NIUWATUAMU**-ni viambishi mahsusi vya Lugha ya Kiswahili Sanifu ambavyo huwakilisha nafsi za watu mbali mbali katika lugha.

Kiambishi mahasusi cha wakati/njeo.

NA	-kiambishi awali wakati uliopo	-a/ na /lima.
ME	- kiambishi awali wakati timilifu	-a/ me /mpeleka.
LI	- kiambishi awali wakati uliopita	-a/ li /mpeleka.
TA	-kiambishi awali wakati ujao	-a/ ta /mpeleka.
HU	-kiambishi awali wakati mazoweya	-/ hu /mpeleka.

Viambishi hivi vya wakati huunda kipashio- **NAMELITAHU**-ambavyo ni viambishi mashuhuri vya Kiswhili Sanifu hivi huwakilisha njeo za nyakati mbali mbali katika lugha. Kama inavyoonekana hapo juu katika tungo hizi fupi kila moja inazungumziwa wakati tofauti na nyingine.

Kiambishi “ka” katika lahaja ya Kipemba

Kiambishi “ka” katika lahaja ya Kipemba kinabeba dhima mbili kuu ambapo dhima hizo hujitokeza katika tungo moja tu; dhima ya kuwakilisha nafsi na dhima ya kuwakilisha wakati (njeo).

Ka +niti /ka/	-kiambishi awali kiwakilishi nafsi ya tatu, umoja, mtenda. -kiambishi awali kiwakilishi njeo ya wakati timilifu.
Ka+oo /ka/	-kiambishi awali kiwakilishi nafsi ya tatu, umoja, mtenda. -kiambishi awali kiwakilishi njeo ya wakati timilifu
Ka+po/ka/	-kiambishi awali kiwakilishi nafsi ya tatu, umoja, mtenda. -kiambishi awali kiwakilishi njeo ya wakati uliopo

4.9 Hitimisho

Sura hii ni mjumuiikowa uchunguzi na afafanuzi wa data za utafiti; ambapo utafiti uliwakusanya jumla ya watafitiwa 42 waliowakilisha kundi kubwa la watafitiwa wenzao, aidha utafiti uligundua matumizi ya kiambishi katika lahaja ya Kipemba, tofauti na uhusiano wa kiambishi kikilinganishwa na viambishi vya Kiswahili sanifu, tofauti za maumbo maneno na uchipuaji wa dhana nyingi katiya lahaja hii na Kiswahili Sanifu.

SURA YA TANO

MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii ni hitimisho la utafiti ambao ulihusu ulinganishaji wa midhihiriko na matumizi ya kiambishi katikalaha ya Kipemba, uliofanywa Kaskazini Mashariki na Kusini ya Kisiwa hicho. Sura hii inahusu Muhtasari wa utafiti kwa ujumla, Muhtasari wa matokeo ya utafiti, Mchango wa utafiti na Mapendekezo ya utafiti huu.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kubainisha matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba. Ili kufikia lengo kuu utafiti ulijikita katika kuyafafanua matumizi ya kiambishi katika viambo mbali mbali vya lahaja hii, misamiati na tungo. Utafiti ulikuwa na malengo matatu; Kuchunguza sababu za kutumia kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba, kubainisha athari za matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba na Kubainisha makundi ya matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba, ambapo malengo haya yalifikiwa, kwa kutumia data zilichangiwa kwa jumla ya watafitiwa washiriki 42. Hawa waliwakilisha kundi kubwa la watafitiwa kwa kujibu maswali 79 ya utafiti wote. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu za mahojiano ya ana kwa ana, dodoso na uchunguzi makini na data hizi zilichambuliwa kwa njia ya maelezo, majedwali yalitumika pale ambapo yalihatijika ili kurahisisha ufahamu.

Ili kuyafikia malengo haya utafiti ulitumia Nadharia ya miundo katika kuviaridhi viambajengo vya maneno katika lahaja husika na ndiyo Nadharia iliyofanikisha kwa kufafanua kiunzi picha cha miumdo ya maneno, kiunzi picha hicho kikionesha

maumbo maneno yalivyotawanyika na yalivyojieka pamoja kuunda lahaja. Kwa hiyo ni wazi kuwa Nadharia hii inaenda sambamba na utafiti huu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kiambishi hushikamana katika kila ngazi.

Utafiti huu uliundwa na sura tano kuu zikiwa na mtiririko mwanana kama huu:-Sura ya kwanza ilitoa taarifa kuhusu mada ya utafiti, vipengele vilivyoielezwa ni kama kiambishi katika lahaja ya Kipemba, Usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na vikwazo vya utafiti.

Sura ya pili ilihusu mapitio mbali mbali ya kazi tangulizi yaliyoandikwa kuhusu mada hii, maana ya lahaja, aina na umuhimu wa lahaja, matumizi ya kiambishi, matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba, Nadharia kuhusu lahaja, Nadharia kuhusu kiambishi, kiunzi cha Nadharia na hitimisho.

Sura ya tatu ilihusu namna utafiti ulivyofanyika ikihusisha muundo wa utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli na hatua zake, mbinu za ukusanyaji data ; usaili, dodoso pamoja na uchunguzi makini, miiko ya utafiti pamoja na hitimisho la sura.

Sura ya nne imewasilishwa na kuchambuliwa data zilizokusanywa kutoka uwandani ili kujibu maswali ya utafiti na kuyafikia malengo yaliyokusudiwa katika utafiti huu.

Sura hii iliundwa na sababu za kutumia “ka” na “ku”, makundi na jinsi za watafitiwa, kuvuka mipaka kimatumizi kiambishi “ka” na “ku”, sababu za kuzuka kiambishi, matumizi, mahusiano, tofauti ya kiambishi ukilinganisha na mofu zingine katika lahaja ya Kipemba.

Sura ya tano ambayo ni yamwisho katika utafiti huu, ni sura iliyotoa muhutasari wa utafiti mzima, muhutasari wa matokeo ya utafiti, mapendekezo, tafiti fuatizi pamoja na hayo sura ya tano imetoa maoni kuhusu tafiti zinazoweza kufanywa ili kuendeleza lahaja ya Kipemba.

5.3 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ambao ulifanyika katika kisiwa kidogo cha Pemba katika maeneo teule yaliyotajwa, matokeo yake yalionesha kuwa watumiaji wa lahaja ya Kipemba wanatumia kiambishi kwa kiwango kikubwa, ripoti hii ilinukuliwa kutoka kwa washiriki wa rika na jinsi tofauti walioshirikishwa katika utafiti huu. Washiriki hawa kwa kiasi cha asilimia 81.5% walioeleza ukweli wa kutumia kiambishi katika lahaja hii. Wasomi na wasiosoma walioshiriki walichangia kueleza matumizi ya kiambishi katika maeneo mbali mbali ya tungo za lahaja ya Kipemba ambapo paliibuka matumizi katika njeo, nafsi, tungo masharti, mafumbo, vitarafa (tungo swali/mshangao) na utamatishaji wa maneno.

5.3.1 Kuchunguza Sababu za kutumia Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba.

Kiambishi hutumika kwa sababu mbali mbali za lahaja ya Kipemba maeneo hayo nipamoja na:-

Sababu utumiaji wa lahaja hio kihistoria, Wapemba hukulia katika mazingira ya jamii ya wazee wao walikuzwa kimaadili, kijamii na huku wakijikuta wamerithi matamshi kutoka kwa wazazi wao.

Sababu nyingine ni kulinda lugha na msamiati katika jamii zao; kila jamii ilikuwa makini kulinda msamiati wa jamii yao. Walilazimika kulinda msamiati wao kwa kutumia lahaja hiyo kwani kulikuwa na haja ya mawasiliano kati yao na wanajamii husika.

Sababu nyingine ni ile iliyodaiwa kuletwa na mtengano wa kijografia, wakaazi wa maeneo mbali mbali walitofautishwa kilahaja na jamii nyingine kutokana na umbali wa kijografia. Wakaazi wakijiji X mathalani walitamkatofauti kiambo fulani ukilinganisha na wakazi wakijiji Y, kutokanana masafa yaliyokuwepo kati ya watu hao wa jamii mbili.

5.3.2 Athari za Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba.

Athari mbali mbali zilipatikana katika msamiati; msamiati mwingi ulionekana kuwa na mawanda mapana ya matumizi ya kiambishi, katika nomino na kitenzi. Athari hizi ziligundulika katika kiambishi kilipotumika katika lahaja ndani ya utafiti huu, yaani kilikuwa na maana:-

Kutokanana njeo.

Kutokanana kiambishi nafsi.

Kutokanana kiambishi tamati.

Kutokanana kiambishi katika mafumbo.

Kutokanana kiambo cha kitarafa.

Kutokanana kiambishi katika tungo ukinzani.

5.3.3 Makundi ya Matumizi ya Kiambishi “ka” na “ku” katika Lahaja ya Kipemba.

Makundi ya matumizi ya Kiambishi yalikuwa na migawanyiko mbali mbali kama yalivyo elezwa katika matokeo ya utafiti huu ambayo ni pamoja na makundi yaliyotokana na;

- Sababu matumizi ya kiambishi kutokana na historia.
- Sababu matumizi ya kiambishi kutokana na kulinda na kuzalisha msamiati.
- Sababu matumizi ya kiambishi kutokana na haja ya mawasiliano.
- Sababu matumizi ya kiambishi kutokana na utengano wa kijiografia.

5.4 Hitimisho

Utafiti huu umechunguza ulinganifu wa midhihiriko na matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba, utafiti uligundua kuwa kiambishi “ka” na “ku” hudhihiri katika njeo, nafsi, mafumbo, vitarafa. Pia katika utafiti huu kulikua na vyanzo vya kiambishi ambavyo vilitajwa kuwa ni pamoja na chanzo cha kijografia, kihistoria, kudumisha lugha na mengineyo ambayo yote haya yalitoa athari zake katika nomino na kitenzi cha lahaja hii.

5.5 Mapendekezo

Baada ya kukamilika kwa utafiti huu kulikua na mapendekezo mbali mbali ambayo yalitolewa na mtafiti kwa nia ya kujenga umakini wa wanalugha. Miongoni mwa mapendekezo hayo nipamoja na:-

Kuitaka jamii ya Wapemba kutumia vilahaja vyao, kuwasiliana bila kuwa na hofu kwani kuizungumza kutasaidia kuipandisha hadhi lahaja hii kubwa ambayo ina mfumo wa vilahaja vidogo vidogo ndani yake.

Kuwataka watu wa ulimwenguni kuzungumza Kipemba, pia kujifunza kwa wale wasio kijua kwani hii ni lahaja yenye mawasiliano kama lugha nyingine, kutumia lugha hii kunafanana na kijilugha chochote duniani, hivyo watumie bila ya hofu.

Kuitaka serikali iipandishe hadhi lahaja hii kwa kuirasimisha ili itumike katika Nyanja za:- elimu tekinolojia na ufundi.

5.6 Tafiti Fuatishi

Utafiti ulipendekeza kuwa ipo haja ya kufanywa tafiti zingine kwani waandishi wengi waliandikia matumizi ya kiambishi katika kiwango cha lugha ya Kiswahili Sanifu. Ambapo kwa upande wa utafiti huu, alichagua lahaja ya Kipemba. Hivyo aliwataka watafiti wafanye tafiti juu ya lahaja ya Kipemba, hasa kuandikia kazi za kiambishi katika lahaja ndogo ndogo zinazozungumzwa Pemba. Kuandikia kiambishi “ka” na “ku” kinavyotumika sambamba na lahaja hii.

MAREJELEO

Adam, J. Kamuzora, F. (2008). *Reasarch Methodology for Bussiness and Social Studies*. Morogoro; Mzumbe Book Project.

BAKIZA. (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Besha, R. (2007). *Mtalaa wa Isimu*. Dar es Salaam: Dar- es-salaam University Press.

Chomsky, N. (1957) *Syntactic Structure Moulon*. Montton: Hang.

Jane Thungu et all, (2010) *Mastering P.T.E. Education*: Nairobi: Oxford University Press.

John, H. & Peter, K. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoneoex Publisher L.t.d.

Kihero, Y. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswhili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Kothari, C. R. (2009). *Research Methodology*. New Delhi: New age International (P) L.t.d.

Kothari, R. (2004). *Research Methodology: Method and Technique*. New Delhi: New age International (P) L.t.d.

Makala. (2014) Majukmu ya Lahaja; PDF

Massamba, D. P. B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*: Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2011). *Isimu Jamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2012). *Misingi ya Fonolojia: Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mathooko, P. M. (2007), *Isimu Jamii: Misingi ya na Nadharia*. Nairobi: Njiko Books.

Matthews, P. H. (1993). *Mofolojia* two (2) Edition. London: Cambridge University Press.

Mdee, J. S. (2010). *Nadharia, Historia na Leksikografia*. Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, R. (2001). *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Alphabetic Company.

Mnata, R. (2014). *Semantiki na Pragamatiki ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Karljama Printer Technology.

Mshindo, H. (1980). "The Use of "ka" In Pemba Swahili Variety." Unpublished M.A Linguistics Desseration of the Univrsity of Dar-es-Salama.

Njoku, K. (2006). *Maana ya Lahaja*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

- Riro, S. (2012). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
- Robinson, H. (1981) *General Linguistic, An Introductory Survey*: Language Group L.t.d.
- Sacleux. (1909). *Grammaire des Dialectals Swahili*. Paris: Frasi.
- Spencer, A. (1919). *Mofological Theory an Introduction to Word Structure In Generative Grammer*. London: Comrage University Press.
- Stigand, C. (1915). "A Grammer of Dialect Change in Kiswahili Language." London University Press .
- TUKI (2004). *Kamusi la Kiswahili Sanifu*. Dar-es-salaam: TUKI.
- Vartanian, T. (2011). *Secondary Data Analysis*. New York: Oxford University Press.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO NA.1: MWONGOZO WA DODOSO LA MASWALI KWA AJILI YA UTAFITI

(LIMETAYARISHWA KWA AJILI YA WASOMI TU)

Dodoso hili ni kwa ajili ya utafiti tu, si kwaajili ya mambo mengineyo kwani mtafiti ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huriya, majawabu yatakayopatikana ni siri kati ya mtafiti na

mtafitiwa.

Jina la mkoa..... Jina la wilaya.....

Jimbo la..... Shehiya

Kijiji cha..... Jina la mtafitiwa(si lazima).....

Bainisha matumizi ya kiambishi katika lahaja ya Kipemba.

1a) Je, kiambishi “ka” na “ku” kinatumika katika Lahaja ya Kipemba?

i. Ndiyo ii. Hapana

(b). Kama jawabu ni ndiyo, taja maneno matatu ambayo kiambishi “ka” na “ku” hutumika katika lahaja ya Kipemba.

i.....ii.....iii.....

2(a) Je, kiambishi “ka” na “ku” kinadhihiri katika makundi yapi ya maneno katika lahaja ya Kipemba?

i.Nomino ii.Kitenzi iii.yote mawili

b) Je, kudhihiri huko kunaweza kuleta athari ya matumizi katika lahaja ya Kipemba ?

i. Ndiyo

ii. Hapana

c) Kama jawabu ni ndio toa maneno mawili uoneshe matumizi tofauti ya kiambishi “ka” na “ku”.

a) Bainisha matumizi ya kiambishi “ku”

i).....i).....

ii).....ii).....

iii).....iii).....

4.(a) Je, kuna sababu zilizopelekea kuzuka kwa kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba?

(b) Taja sababu moja tu

5.(a) Je, kuna athari yoyote inayojitokeza katiak lahaja ya Kipemba kutokana na kiambishi “ka” na “ku” ?

(b) Taja athari moja unayoielewa.....

6 (a) Fafanua kwa ufupi matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba ukilinganisha na viambishi vingine katika Kiswahili Sanifu.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

KIAMBATANISHO NAMBA 2: HOJAJI KWA WATAFITIWA WASOMI TU

1(a) Je, kuna dhana tofauti ya maumbo (kiambishi) katika lahaja ya Kipemba na Ks. Sanifu?

Ndiyo

Hapana

(b) Kama jibu ndiyo toa misamiati miwili inayo kiambishi “ka” na “ku” katika kila lugha.

i.....

ii.....

iii.....

iv.....

(c) Eleza kwa ufupi dhima za kila kimoja katika kiambishi ulicho taja.

i.....

ii.....

iii.....

iv.....

2. a) Je, kuna mfanano wa matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” kati ya Ks. Sanifu na lahaja ya Kipemba?

i- Ndio

ii-Hapana

(b) Kama jibu ni ndio taja mfanano huo upo katika nini?

i- Viambishi njeo

ii-Kiambishi nafsi

iii-Yote mawili

(c) Toa mfano wa neno moja kuthibitisha kauli yako.

.....

4. Taja tofauti za kiambishi “ka/ku” kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili Sanifu.

.....
.....

5. Je, kuna athari yoyote katika lahaja ya Kipemba inayotokanana kiambishi “ka” na “ku” ?

i- Ndio ii- Hapana

6. Tunga sentensi mbili kuthibitisha jibu lako.

i.....

ii.....

KIAMBATANISHO NAMBA 3: MWONGOZO WA USAILI

KWA AJILI YA UTAFITI

(LIMETAYARISHWA KWA AJILI YA WASIOSOMA TU)

Dodoso hili ni kwa ajili ya utafiti tu, si kwaajili ya mambo mengine kwani mtafiti ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huriya, majawabu yatakayopatikana ni siri kati ya mtafiti na mtafitiwa.

Jina la mkoa..... Jina la wilaya.....

Jimbo la..... Shehiya

Kijiji cha..... Jina la mtafitiwa (si lazima).....

SEHEMU-A

Bainisha matumizi ya Kiambishi katika lahaja ya Kipemba.

1a) Je, kineno (kiambishi) “ka” na “ku” kinadhihiri katika lahaja ya Kipemba?

i. Ndiyo ii. Hapana

b) Kama jawabu ni ndiyo taja maneno matatu ambayo yana (kiambishi) “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba.

i.....ii..... iii.....

2a) Je, kuna matumizi ya kiambishi zaidi katika lahaja ya Kipemba kuliko viamishi vya Kiswahili Sanifu?.

i)Ndiyo (ii) Hapana

b) Kama jibu ni ndiyo, taja maneno matatu kuthibitisha jibu lako.

i)..... (ii)..... (iii).....

c) Taja sababu moja ya kuzuka kwa kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba. i.....

3a) Je, kiambishi “ka” na “ku” kinajitokeza katika mafumbo?

i-Ndio

ii- Hapana

c) Kama jibu ndio lete mafumbo manne yenye kiambishi “ka” na “ku” kuthibitisha jibu lako.

i.....

ii.....

iii.....

iv.....

4a) Je, kiambishi “ka” na “ku” kinaweza kutumika kuunda maswali katika lahaja ya Kipemba.

i-Ndio

ii- Hapana

b) Kama jibu ndio lete maneno mawili kuunda maswali kwa kila kiambishi kimoja.

i.....

ii.....

iii.....

iv.....

SEHEMU-B

Kiambishi hujitokeza katika tungo masharti; angalia mifano hii kisha bainisha kwa kupigia mstari chini yake.

Mfano:- Akumwilikaye mchana usiku akuchoma.

-Akutukanaye hakuchagulii tusi.

-Akulaumuye akupenda.

-Akufaaye kwa dhiki ndiye wako rafiki.

-Akufukuzaye hakuambii toka..

-Udugu nikufaana udugu sikufanana.

-Ukuu kuu wa kamba si upya wa ukambaa.

-Kutangulia sikufika.

-Kutembeya nikusoma.

b) Je, kuna tungo nyingine ambazo unadhani kiambishi hutumika? eka✓ au x

i-Ndio

ii- Hapana.....

iii-Kama jibu ndio toa mifano mitatu tu.

a

b.....

c.....

2. Kiahimbishi hujitokeza katika mafumbo.mifano;

Ukubwa ni jaa.

Umoja ukulani.

a) Toa mifano mitatu unayojua iliyo na kiambishi ku katika mafumbo.

i).....

ii).....

iii).....

b) Kiahimbishi ka kinavyojitokeza katika mafumbo.

Kawiya ufike.

Kauli ya mama

Toa mafumbo mitatu unayoyajua yaliyo na kiambishi ka.

i).....

ii).....

iii).....

**KIAMBATISHO NAMBA 4: MAJIBU YA DODOSO KUTOKAKWA
WALIOSOMA TU**

Dodoso hili ni kwa ajili ya utafiti tu, si kwaajili ya mambo mengineyo kwani mtafiti ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu Huriya na majawabu yatakayopatikana ni siri kati ya mtafiti na mtafitiwa.

Bainisha matumizi ya kiambishi “ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba.

- 1a) Je, kiambishi“ka” na “ku”kinadhihiri katika lahaja ya Kipemba?
i. Ndiyo ✓ ii. Hapana
- (b) Kama jawabu ni ndiyo, taja maneno matatu ambayo yana kiambishi“ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba.
i- kamo ii kuji iii kapo
- 2a) Je, kiambishi“ka” na “ku” kinadhihiri katika aina gani ya maneno katika lahaja ya Kipemba?
i.Nomino ii.Kitenzi iii.yote mawili.....✓
- b) Je, kudhihiri huko kunaweza kuvuka mipaka ya matumizi ni(zaidi ya K. Sanifu)?
i. Ndiyo ✓ ii. Hapana
- c) Kama jawabu ni ndio toa maneno matatu uoneshe matumizi tofauti ya kiambishi“ka” na “ku”.
i- kalale ii kuono? iii kanijuu
ka-nafsi ya tatu umoja ku-nafsi ya pili umojaka-nafsi ya tatu umoja

ka- amri

ku-mtendaka-mtenda

ka-wakati uliopo

ku- wakati uliopo ka-wakati uliopo

4a) Je, kuna sababu zilizopelekea kuzuka kwa kiambishi“ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba?

b) Kamaiko taja moja tu

Sababu za mtawanyiko wa watu katika jamii za Wapemba.

5a) Je, kuna athari yoyote inayojitokeza katiak lahaja kutokanana kiambishi“ka” na “ku” ?

b) Taja athari moja unayoielewa.

Athari katika msamiati ndani ya njeo.

**KIAMBATANISHO NAMBA 5: MAJIBU YALIYOTOLEWA KUTOKANA
NA HOJAJI KWA WASIOJUA KUSOMA**

- 1a) Je, kineno(kiambishi)“ka” na “ku” kinadhihiri katika lahaja ya Kipemba?
i. Ndiyo ✓ ii. Hapana
- b) Kama jawabu ni ndiyo taja maneno matatu ambayo yana(kiambishi)“ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba.
i- kalaleni ii kakuuka iii kanioni
- 2a) Je, kuna matumizi ya kiambishi zaidi katika lahaja ya Kipemba kuliko viamishi vya Ks. Sanifu?. i)Ndiyo ✓ (ii) Hapana
- b) Kama jibu ni ndiyo, taja maneno matatu kuthibitisha jibu lako.
(i) kalinae (ii) kupo . (iii) kamuoo
- c) Taja sababu moja ya kuzuka kwa kiambishi“ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba.
i- kila jamii ina kilahaja chake katika eneo lake.
- 3a) Je, kiambishi“ka” na “ku” kinajitokeza katika mafumbo?
i-Ndio ✓ ii- Hapana
- b) Kama jibu ndio lete mafumbo manne yenye kiambishi“ka” na “ku” kuthibitisha jibu lako.
i- kufa nkufaana ii- umoja ukulani
iii- kukopa harusi iv kapu la mwinyi
- 4a) Je, kiambishi“ka” na “ku” kinaweza kutumika kuunda maswali katika lahaja ya Kipemba. i-Ndio ✓ ii- Hapana
- b) Kama jibu ndio lete maneno mawili kuunda maswali kwa kila kiambishi kimoja. i- Kumbe ?ii- Kamwe ?iii- Akaa ? iv- Kumbee ?

KIAMBATISHO NAMBA 6: BAADHI YA MSAMIATI WA LAHAJA YA**KIPEMBA**

KI-Kipemba	Ks- Sanifu
Kuji	Umekuja
Kuvuni	Umevuna
Kalimi	Halimi
Kwendi	Huendi
Ka!	Akaa!
Eka	Weka
Kurudi	Umerudi
Kefika	Hakufika
Kakipo	Hakipo
Kawapo	Hayupo
Kalipo	Halipo
Kiwapo	Kipo
Kiji	Kimekuja

MAJIBU YALIYOTOLEWA KUTOKANA NAHOJAJI KWA WASOMI TU

- 1a) Je, kuna dhana tofauti ya maumbo (kiambishi) katika lahaja ya Kipemba na Ks. Sanifu? Ndiyo ✓ Hapana
- b) Kama jibu ndiyo toa misamiati minne yenye kiambishi“ka” na “ku” katika lahaja ya Kipemba.
- i- kuntukimbia ii- kizuka
- iii- kali nami iv -kaamini
- c) Eleza kwa ufupi dhima za kila kimoja katika kiambishi ulicho taja.
- i- dhima ya nafsi ii- dhima ya kukamilisha maana
- iii dhima ya nafsi iv- dhana ya njeo
- 2a) Je, kuna mfanano wa matumizi ya kiambishi“ka” na “ku” kati ya Ks. Sanifu na lahaja ya Kipemba? i- Ndio ✓ ii-Hapana
- b) Kama jibu ni ndio taja mfanano huo upo katika nini?
- (i) Viambishi njeo (ii) Kiambishi nafsi (iii) Yote mawili ✓
- c) Toa mfano wa neno moja kuthibitisha kauli yako.
- A-ku-ambiyaKu- yadokeza urejeshi.
4. Taja tofauti moja ya kiambishi ka/ku katika lahaja ya Kipemba na viambishi vya Ks. Sanifu.Kiambishi“ka” na “ku” ina dhima ya njeo, nafsi, umoja, wingi, mtenda, mtendwa, urejeshi nk.
- 5a) Je, kuna athari yoyote katika lahaja ya Kipemba inayotokanana kiambishi“ka” na “ku” ?
- i- Ndio ✓ ii- Hapana
- b) Tunga sentensi mbili kwa kuthibitisha jibu lako.
- i- kamba ndefu haifungi kuni ii kuimba kunajenga haiba

KIAMBATISHO NAMBA 7: Msamiati ulioonesha kuchupa mipakakwa “ka naku” katika lahaja ya Kipemba

Msamiati	Kazi mbali mbali za “ka naku”
Kuji	/ku/+ mpumuo, iliwakilisha nafsi ya pili, wakati ujao
Kusvuni	/ku/-mpumuo, iliwakilisha nafsi yapili, wakati uliopita
Kalimi	/ka/+mpumuo, iliwakilisha nafsi yatatu, wakati mazoea
Kwendi/kuendi	/ku/-mpumuo, iliwakilisha nafsi yapili, wakati ujao
Ka!	/ka/mshangao, iliwakilisha nafsi (kiwakilishi/mofu jina)
Eka	/ka/-mpumuo, kiambishi tamati maana.
Kurudi	/ku/+mpumuo, iliwakilisha nafsi yapili, wakati ujao.
Kefika	/ka/ tamati maana.
Kakipo	/ka/+mpumuo, iliwakilisha nafsi yatatu, wakati uliopo
Kawapo	/ka/+mpumuo, iliwakilisha nafsi yatatu, wakati uliopo.
Kalipo	/ka/+mpumuo, iliwakilisha nafsi yatatu, wakati uliopo.